Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika Wake humsalia Mtume; enyi mlioamini, msalieni (Mtume) na mwombeeni amani.
Kwa yakini wale wanaomwudhi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, Mwenyezi Mungu Amewalaani katika dunia na Akhera, na Amewaandalia adhabu ifedheheshayo.(33:57-58)

JUZU 75 No. 187 | SAF./RAB1. 1438 AH | NOV./DIS. 2016 | NUB./FAT. 1394 HS | BEI TSH. 500/=

Khalifa Mtukufu atangaza mwaka wa 83 wa Tahrik Jadid:

Tanzania yaingia kumi bora Afrika

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alitoa hotuba katika msikiti wa Baitul Noor, Calgary, Canada, ambapo alitangaza mwaka Mpya wa 83 wa Tahrik Jadid.

Baada ya *Tashahhud* na *Surat Fatihah* Huzur (atba) alisema Masih Aliyeahidiwa(a.s) katika wakati fulani alipotupa mwanga juu ya kujitolea mali alisema katika dunia hii mwanadam anapenda sana mali ndio maana ikaandikwa katika kitabu cha fasiri za njozi kuwa ikitokea mtu akaota anatoa ini lake katika njozi hii inamaanisha kwamba atatoa mali yake.

Ndio maana ikaelezwa ya kwamba ili mtu afikie mafanikio ya kweli na imani ni lazima ajitolee mali yake. Imeelezwa ndani ya Kurani "Hamtaufikia wema hasa mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda". Ni kwa sababu ukarimu na huruma juu ya viumbe vya Allah ni jukumu lingine kubwa la Muaminio ambalo bila ya hilo Imani haiwezi kuwa kamili na thabiti.

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masih V a.t.b.a.

Na kama mtu hakujitolea kiukweli, je kuna njia yoyote ya mtu kuwanufaisha wengine? Kwa ajili ya kuwanufaisha na kuwahurumia wengine, kujitolea ni jambo la lazima. Na katika Aya hii ya: "Hamtaufikia wema hasa mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda", muongozo na mafundisho yanapatikana. Hivyo kutoa katika njia ya Allah pia ni kigezo na ni wajibu wa mtu katika safari hii ya UchaMungu wa mtu.

Huzur (atba) alisema: Nitasoma nukuu nyingine ya Masih Aliyeahidiwa(a.s) ambayo alisema: "Kukubaliwa mbele ya Allah ambapo kiuhalisia ni sababu ya kupata ile furaha ya kweli hakuwezi kufikiwa mpaka mtu avumilie shida siziso za kudumu. Kisha akasema waliobarikiwa ni wale ambao kwa kumthibitisha Mungu Mwenyezi hawajali juu ya maumivu ya muda mfupi kwa sababu imani yao imewapa mwanga wa furaha ya kweli na wanaendelea kupata utulivu baada ya shida za muda mfupi.

Huzur (atba) alisema watu wa leo hii wanafikiri kuwa kurundika mali na kutumia kwa ajili ya haja zao na mahitajio yao inaweza kuwa chanzo cha kupata raha na kupata utulivu. Lakini mweye Imani ni yule anayetambua na aliyekuwa na ufahama wa dini kuwa Mungu Mwenyezi ameumba vitu na mahitajio ya Mwanadamu katika dunia hii lakini lengo halisi la maisha ya binadamu ni kupata ukaribu na Mungu Mwenyezi. Na kukanyaga katika njia ya Ucha Mungu na kutoa haki ya Allah na haki ya viumbe wake. Mungu Mwenyezi amelizungumzia jambo hili katika Aya ya Qurani tukufu niliyoisoma hapo awali. Masih Aliyeahidiwa(a.s) alisema utulivu wa kweli unapatikana kwa kufanya vitendo vyema na sio kurundika mali. Matendo mema hayataweza kukubaliwa hadi mtu atoe vile anavyovipenda katika njia ya Allah na kwa ajili ya manufaa

Endelea uk. 3

Jalsa Salana ya 47 Tanzania yazidi kung'aa

Watu wapatao 3,300 wahudhuria

Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu, Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Tanzania imefanikiwa kufanya Jalsa yake ya 47 mwaka huu kama ilivyokuwa katika miaka mingi iliyopita. Jalsa ilianza tarehe 30 September na kumalizika tarehe 2 Oktoba huko Kitonga, wilaya ya Ilala nje kidogo ya jiji la Dar es salaam

Kama ilivyo kawaida wageni waliokuja kuhudhuria Jalsa walimiminika kutoka mikoa, wilaya, vijiji mbalimbali nchini na nje ya Tanzania. Nchi hizo ni pamoja na Uganda, Malawi na Msumbiji. Wageni hawa walianza kuwasili tangu tarehe 28 ya Mwezi Septemba na taratibu zilikuwa ziko tayari ili kuwapokea na kuwafikisha eneo la Jalsa huko Kitonga. Mkazo pia uliwekwa kuwa ni vyema kwa wajumbe hao wa Jalsa wakaenda moja kwa moja Kitonga badala ya kupitia Mnazimmoja ambapo kwa sasa hakuna nafasi ya kutosha kutokana na harakati za ujenzi wa Msikiti zinazoendelea.

Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akitoa hotuba wakati wa Ufunguzi wa Jalsa Salana 2016

Kamati mbalimbali ziliundwa ili kufanikisha shughuli hii adhimu, miongoni mwa kamati hizo ni pamoja na kamati za chakula, ulinzi, usafi, habari, kupokea wageni n.k. Siku tatu tu kabla ya Jalsa kuanza, Amir na Mbashiri Mkuu alikutana na kamati zote hizi huko Kitonga ili kufanya tathmini ya mwisho ya utekelezaji wa majukumu yote ya kamati na idara zake mbalimbali. Alitoa maelekezo na ushauri kwa baadhi ya kamati na idara pale ilipobidi kufanya hivyo na sehemu nyingine ambazo aliona ziko sawa alishauri wahusika wafanye zaidi ili kujiimarisha zaidi katika kamati na idara zao.

Kama kawaida wageni wote waliohudhuria walitakiwa kufanya usajili mwanzoni kabisa kwenye lango kuu la kuingia kwenye viwanja vya Jalsa, wageni walisajiliwa hapo na kupewa vitambulisho maalum vinavyowatambulisha wao ni akina nani, wametoka katika jamaat gani, umri na jinsi zao. Zoezi hili ni muhimu kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu za wahudhuriaji na hatimae kujua idadi kamili ya mahudhurio.

Idara ya chakula ni moja katika idara ngumu na muhimu sana, idara hii hasa ina jukumu la kuhakikisha chakula kinakuwa tayari kwa wakati pia kuhakikisha kila mtu anapata chakula chake pia kwa wakati. Hakika hapa kuna kazi nyingi sana, ni adara inayohitaji nguvu kazi kubwa

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

TJIFUNZE NDANI YA MSIBA HUU

Tarehe 15/11/2016 siku ya Jumanne, Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania kwa ujumla ilipata msiba mkubwa kwa kuondokewa na Mbashiri shupavu na Sheikh mahiri Salehe Mbaruku Kapilima. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.

Maisha ya Sheikh Salehe Mbaruku Kapilima ni kioo kwetu. Ni maisha ambayo tunayo mengi ya kujifunza. Sheikh Salehe alikuwa mtafutaji mzuri wa elimu. Alitembea nchi nzima akitafuta elimu. Alijikusanyia kwa gharama yoyote kila kitabu cha maana alichokiona. Ari hii inatakiwa sana kwa hivi sasa kwani kuna mambo mengi ya kujifunza na bahari ya elimu ni ile iliyoletwa na Masihi Aliyeahidiwa Seyidna Ahmad a.s. Tunayo bahati kubwa ya kuwa na vitabu vya mjumbe wa Allah katika Kiswahili.

Tunatakiwa kufanya jitihada ya kuvisaka na kuvisoma. Nusura yetu itapatikana kwa kutumia njia hiyo. Hakuna njia nyingine ya kunusurika na haya yanayotukabili hivi leo isipokuwa kujisomea elimu kutoka chuo cha Mwana huyu wa kiroho wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. yaani Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s.

Sifa ya pili aliyokuwa nayo Sheikh Salehe ni kusambaza elimu aliyoipata kwa wengine. Hii ni dalili ya kutokuwa na uchoyo. Popote alipokwenda jukumu lake la kwanza ilikuwa kuanzisha darasa. Wale aliowafundisha wanamsifu kwa unyenyekevu wake na jazba ya kutoa elimu. Hakuonyesha majivuno ya kujua bali alikubali siku zote kwamba mwalimu mzuri ni yule pia aliyekuwa tayari kuwa mwanafunzi mzuri. Aliwasikiliza wanafunzi wake na kubadilishana nao mawazo. Kila alipofundisha aliacha athari kubwa.

Lakini burudani ya moyo wake ilikuwa ni kuhubiri, na hii ni sifa yake nyingine. Alipenda sana kufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Alikuwa ni mhubiri asiyekuwa na papara na asiyechoka. Hakuwa na haraka. Alijaribu kuyaelewa mazingira kwanza na hivyo kuhubiri sawa na haja. Kuhubiri kunahitaji hekima kubwa. Na ndivyo alivyofanya huko Rufiji. Mara alipoukubali ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. na kuamua kuufikisha kwa jamaa zake, hakufanya haraka ya kuwaeleza ujaji wa Masihi. Aliona walitakiwa kwanza kufahamu vitu vingine vingi. Na alifanya hivyo. Alikuwa ni mkulima nzuri. Alitayarisha ardhi, akaweka mbolea na alipopanda mbegu zikaota kwa haraka na kutupatia matunda matamu - Waahmadiyya hodari.

Sheikh Salehe Mbaruku Kapilima alikuwa ni kamusi ya historia ya Ahmadiyya nchini. Kafanya kazi na masheikh wengi. Katafuta viwanja vingi vya Jamaat kikiwemo cha Msikiti wa Dar es Salaam na Morogoro. Mambo mengi muhimu kuhusu Jumuiya yeye aliyaona na kushiriki. Alijuana takriban na Waahmadiyya wote wa mwanzoni, wakati mwingine alifunga safari ya kutoka mkoa mmoja hadi mwingine kwa lengo la kumtembelea ndugu yake Ahmadiyya aliyesikia kuwa yuko huko. Aliyakumbuka mambo na matukio kadhaa ya Jamaat kwa siku na tarehe. Ukiwa na watu wa namna hii historia yenu katu haipotei.

Tunalo la kujifunza katika hilo. Tujivunie historia yetu na tuihifadhi na kuiheshimu na hiyo ndio njia bora ya kumuenzi Sheikh Salehe Mbaruku Kapilima kwa kazi kubwa aliyoifanyia Jamaat.

Mwenyezi Mungu Apokee utumishi wake kwa mikono miwili, Amlipe malipo mema yenye kuheshimika na Akisaidie kizazi chake cha kimwili na kiroho kukanyaga pale alipokanyanga yeye, ili nasi tuwe wanafunzi wake wema na warithi wake wema. Amin.

Jalsa Salana ya 44 Tanzania yazidi kung'aa

Kutoka uk. 1

zaidi. Hadi wameweza kufanya kazi na kutimiza majukumu yao tena kwa wakati. Ni idara inayoanza kazi mapema sana na kila mara huwa ya mwisho kumaliza kazi zake.

Kama ilivyo utamaduni wetu, Ijumaa ambayo ndio ufunguzi wa Jalsa hufanyika, kunakuwa na hotuba kadhaa, ikiwepo khotuba ya Khalifatul Masih ambayo inafuata baada ya hotuba ya swala yetu ya Ijumaa na chakula. Baada ya kumaliza ratiba hizo wajumbe wakakaa kusikiliza hotuba ya Khalifatultul Masih V (a.t.b.a). Katika hotuba yake pamoja na mambo mengine, alitutakia Jalsa njema na yenye mafanikio huku akisisitiza sana umuhimu wa mapenzi katika nchi, yaani kuipenda nchi yako ni sehemu ya Imani, hivyo alisisitiza kuwa wanajumuiya wote kwa kujua na kutenda hili wajue kuwa wanatimiza wajibu wao ambao huwa na malipo yake kwa Mwenyezi Mungu kwa kuwa na mapenzi ya dhati kwa nchi zao. Aliendelea kusisitiza kuwa ni muhimu kutii serikali zilizoko madarakani na kuwa hiyo inakwenda sambamba na mapenzi kwa nchi. Aidha aliwaasa wanajumuiya kutojiingiza katika migogoro ya aina yeyote katika nchi zao, na kuwa wao ndio wawe mfano wa kuigwa miongoni mwa raia wa nchi zao. Hotuba hiyo iliyosikilizwa na wahudhuriaji wote wakiwa chini na kwa umakini mkubwa na kubwa zaidi waliweza kusikia moja kwa moja katika lugha ya Kiswahili.

Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu mkutano ulifunguliwa na Naibu waziri wa mambo ya Ndani ya nchi ndugu Hamad Yusuf Masauni Mb ambae alisema kuwa anafurahishwa sana na nidhamu kubwa iliyopo katika Jumuiya hii, alisema kuwa hajawahi kusikia kuwa wanajumuiya wamejihusisha na jambo lolote linalokwenda kinyume na maadili ya nchi kwa ujumla wake.

Mh. Masauni alisema kuwa yeye amekuwa akiifuatilia Jumuiya kwa muda mrefu sana, ingawa hajawahi kuhudhuria kwenye mikutano ya jumuiya lakini alikiri kuwa kuwepo kwake kipindi hiki, amejifunza mengi kutoka kwa wanajumuiya.

Kwa mara ya kwanza katika historia ya Jumuiya hasa katika mikutano ya Jalsa na hii ikiwa ni Jalsa ya 47 mwaka huu tuliweza kuwa na mgeni rasmi Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili Alhaji Ally Hassan Mwinyi, ambae amekuwa akialikwa mara kadhaa lakini mwaka huu kwa fadhila za Mwenyezi Mungu aliweza kufika katika Jalsa. Katika salamu zake, mzee Mwinyi alisisitiza sana juu ya umuhimu wa amani miongoni mwa Jamii za kiislam, na kuwa mifarakano si mizuri kwani inarudisha nyuma maendeleo ya watu. Alipongeza sana jumuiya kwa kufanikisha mkutano huo mkuu wa mwaka na kusema hilo ni jambo zuri kwa Waislam kukutana na kukumbushana mambo mbalimbali ya kidini kama ilivyosisitizwa sana na Mtume wetu mtukufu (S.A.W). Rais huyo Mstaafu, Ally Hassan Mwinyi alisema amefurahishwa kwa mjumuiko huo wa wananjumuiya kutoka sio tu Tanzania bali hata kutoka nje ya Tanzania, akitaja nchi za Msumbiji, Uganda, n.k.

Sehemu ya washiriki kwenye Jalsa Salana 2016

Katika siku 3 za mkutano huo, mambo mbalimbali yalizungumzwa, hotuba za aina mbalimbali zilitolewa zenye mafunzo na zenye elimu ya kina kuhusu dini tukufu ya Islam na ujumbe wa Masih Aliyeahidiwa. Miongoni mwa hotuba zilizofana sana ni pamoja na hotuba ya Sheikh Athumani Kambaulaya, ambayo hasa ilizungumzia swala zima la Taqwa na ucha Mungu. Ilikuwa ni hotuba iliyosisimua washiriki wengi katika mkutano huo, kiasi hiki kwamba baadhi ya watu waliomba mara baada ya Jalsa kupatiwa nakala ya hotuba hiyo. Sheikh alisema mengi lakini kubwa hasa ni ile yakini ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na kuwa tunapofanya maombi tuwe na yakini kuwa maombi yetu tunayapeleka kwa Mwenyezi Mungu ambae ni yeye tu mwenye uwezo wa kutatua shida zetu.

Pia kulikuwa na hotuba nzuri iliyokuwa na ujumbe wa swala zima la Ibada ya Hijja iliyotolewa na Alhaji Abdulrahmani Ame. Itakumbukwa kwamba mwezi mmoja kabla Mwl. Ame alitimiza nguzo ya Tano ya ibada ya Hija. Wengi walivutika mno na hotuba hii pia kwani kama sote tunavyofahamu umuhimu wa kwenda kuhiji. Hivyo wajumbe wengi waliweza kusikia hotuba hii ambayo iliamsha ari kubwa ya wanajumuiya kufanya juhudi za kutekeza ibada hii muhimu. Inshaalah.

Kwa kuwa jumuiya imepata mafanikio makubwa hapa Tanzania kwa kupata wanajumuiya wengi waliojiunga na jumuiya kutoka katika mikoa ya Shinyanga, Mwanza na Simiyu na Tanzania nzima kwa ujumla wake, hivyo kuliwekwa kipindi maalum cha watu kutoa ushuhuda wa jinsi walivyoitambua na kujiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya. Kipindi hiki kilifurahiwa na watu wengi, kwani sehemu kubwa ya waliotoa ushuhuda walizungumzia visa na mikasa iliyowakuta nayo.

Siku ya mwisho ya Jalsa tulipata mgeni rasmi ambaye ni Meya wa jiji la Dar es Salaam. Mstahiki Isaya Mwita. Akitoa salama zake katika Jalsa hiyo, mstahiki Meya huyo aliwaasa vijana kutafuta elimu na kufanya kazi kwa bidii kadiri wanavyoweza, kwani msingi mkubwa wa maendeleo unatokana na elimu iliyoachwa kwa vijana na wazee waliopo katika jamii.

Alisema inasikitisha kuona vijana wanakuwa na kuendelea kukaa tu nyumbani kwa baba na mama hata baada ya kuwa na familia yake.

Katika kumalizia Jalsa salana hiyo, kulikuwa na utoaji wa zawadi kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao katika ngazi mbalimbali, kuanzia shule za msingi mpaka ngazi za vyuo vikuu, zoezi hili lilifanywa na Amir na Mbashiri mkuu Sheikh Tahir Mahmood Choudhry akishirikiana na afisa kutoka ubalozi wa Pakistan ambae alikuwepo hapo kama mgeni mualikwa.

Baada ya zoezi hilo, kulikuwa na hotuba ya ufungaji wa Jalsa salana, iliyotolewa na Amir na Mbashiri mkuu, ambaye alisisitiza sana swala la utii na kufuata nidhamu ya Jumuiya. Sheikh Tahir Mahmood Chaudry alisema kuwa mwaka huu mahudhurio yalikuwa mazuri ukilinganisha na mwaka jana, ambapo kwa mwaka huu wahudhuriaji walikuwa takribani watu 3300.

Baada ya hotuba hiyo, Jalsa ilifungwa kwa maombi ya kimya yaliyoongozwa na Amir na Mbashiri mkuu.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Tanzania yaingia kumi bora Afrika

Kutoka uk. 1

ya viumbe wake. Masih Aliyeahidiwa(a.s) alisema mali ni kitu ambacho mwanaadamu anakipenda sana.

Huzur (atba) alisema ikiwa leo tutatazama kwa makini hali ya dunia basi tutagundua kuwa katika kila magomvi, hofu na usumbufu unaojitokeza katika dunia basi nyuma yake kuna huba na tamaa ya kupenda mali. Kisha Huzur(atba) akaeleza, jambo lingine ambalo watu wa kidunia hawalijui ni kwamba ikiwa amerundika mali nyingi, Je ni njia gani ya kuitumia mali hiyo?

Katika nchi za Magharibi ambazo wanaziita nchi zilizoendelea kuna matajiri wa hali ya juu sana lakini wanafanyaje kwenye matumizi yao? Hapa wana maeneo kama Makasino ambapo wanafuja mali zao kwa matumizi ya kujifurahisha na kucheza kamari. Nchi za kiislam nazo zina hali hiyo hiyo, waislam wanakuja katika nchi hizi kufuja mali zao kwa matumizi ya kujifurahisha. Hivi sasa nchi za kiislam zina sehemu ambazo wanatumia fedha zao kupita kiasi. Huzur (atba) alisema katika siku zilizopita katika safari yangu niliona bango la Ice cream katika Hotel moja huko Dubai. Bei iliyotangazwa ya Ice cream ni Dola 850, ambayo ndani ya Ice cream hiyo kuna vitu vitatu au viwili tu. Walisema ndani yake kuna Zafarani ya sehemu mbalimbali na imefunikwa kwa mfuniko wa dhahabu. Huzur(atba) alisema Dola 850 inatosha kwa maisha mazuri katika familia za nchi maskini lakini watu hawa wanatumia kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kununua kikombe cha Ice cream.

Wale ambao wana mali za kutosha na hawajui namna gani ya kuzitumia na namna gani ya kupata utulivu kupitia fedha zao, haina shaka wanatumia lakini wanafanya kwa ajili ya kukidhi matakwa yao na anasa tu, na sio kwa ajili ya matakwa ya Allah au matendo mema. Lakini maneno ya Mungu Mwenyezi na Masih Aliyeahidiwa(a.s) yalieleza kuwa kwa ajili ya kupata maendeleo na kwa ajili kuongeza imani na kwa ajili ya kutafuta imani na kwa ajili ya kupata radhi ya Mungu Mwenyezi, na kwa kukuza imani, badala ya kutumia mali kwa ajili ya tamaa zao na anasa wanatakiwa kutumia kwa kuwahurumia na kuwafanyia ihsan viumbe vya Mungu Mwenyezi. Ikiwa sio kwa sababu hii basi mtu hawezi kupata mapenzi ya Mungu Mwenyezi. Ili kuwahurumia viumbe vya Allah ni muhimu sana kutimiza mahitajio ya kimwili kwa wanaohitaji, hili ni muhimu kwa ajili ya kulinda hali zao za kiimani na kuwafanya wapate ukaribu na Mungu Mwenyezi.

Huzur(atba) alisema Mtukufu Mtume Muhammad(s.a.w) alikuwa ana hofu juu ya watu wake na imeelezwa ndani ya Quran tukufu pale Mungu Mwenyezi aliposema "Je utajiangamiza nafsi yako kwa kusikitikia hali yao." Je ni hali gani ya watu hawa ambayo ilimfanya awe na hofu juu yao? Ni kwa sababu ya hali yao ya kujitenga na Mungu Mwenyezi na kujitenga na Imani.

Mtukufu mtume Muhammad(s.a.w) alihofia kwa sababu ya jambo hilo pia wanaweza kukasirikiwa na Mungu Mwenyezi kwa kutomuamini. Zaidi ya kupata ufaulu wa mambo ya kidunia, kwa Waahmadiyya ni muhimu kutumia mali zao ili kupata ufaulu wa mambo ya kiroho. Kwa sababu kwa hivi sasa jukumu la kukamilisha muongozo amekabidhiwa Masih Aliyeahidiwa(a.s), muongozo ambao Mtume Muhammad(s.a.w) aliuleta kwa ajili ya walimwengu wote na ambao alipata mashaka juu ya kuenezwa kwake. Katika wakati huu ambao kuna kila njia za kuuneza ujumbe huu. Huzur(atba) alisema kama jukumu hili alivyokabidhiwa Masih Aliyahidiwa(a.s) vile vile kwa sasa jukumu hili wamekabihiwa wafuasi wake. Pia limekabidhiwa kwa wale wanaosema kuwa wanatanguliza dini juu ya dunia.

Watu matajiri wanatumia fedha zao kwa kukidhi haja zao, wana mali nyingi sana kiasi ya kwamba hawajui ni sehemu gani na namna gani wazitumie. Baada ya kutimiza haja zao na mahitajio yao hawajui ni sehemu gani wakatoe kiasi cha fedha kilichobakia. Hali zao za kiroho na kibinadamu ni tupu kabisa, kiasi ya kwamba hawajui kitu kingine chochote isipokuwa tamaa za nafsi zao na upuuzi. Lakini wenye imani ni wale ambao, kuwahusu hao Mungu Mwenyezi anasema sio tu wanatoa mali zao za ziada bali pia ili kupata vitendo vyema na kupata mapenzi ya Mungu Mwenyezi wanajiweka katika hali ya tabu na wanatoa katika mali zao kile wanachokipenda.

Ijapokuwa wapo baadhi ya matajiri ambao pia wanatoa misaada kwa ajili ya maskini lakini misaada wanayoitoa ni midogo sana ukilinganisha na uwezo wao. Na pia hawatoi mara kwa mara. Hivyo, ni yule mwenye Imani tu anayeweza kutoa mara kwa mara ili kupata matendo mazuri. Na katika zama hizi ni jamaat Ahmadiyya tu ambayo ina kundi la waaminio wanaotoa kwa utaratibu na wanatoa kwa ajili ya kusambaza Uislam. Wanatoa katika vipengele mbalimbali. Wanatoa kwa ajili ya kusambaza Uislam na kwa ajili ya kuwahurumia viumbe wa Allah, ambapo wanaona hiyo kuwa wajibu wao kutoa kwa ajili ya wengine. Na pia kuna wengi ambao wanatoa kwa kujiweka katika tabu. Wanatoa katika dhana hii ya kwamba wapate ukaribu na Mungu Mwenye Enzi na wapate Baraka zake hapo ndipo wanaona kwamba wametoa katika haki. Hata wasio kuwa Waahmadiyya wanakubali kuwa mfumo wa kujitolea fedha ndani ya jamaat ni bora.

Huzur(atba) alisema kuna mbashiri wetu kutoka Kababir aliniandikia kuhusu tukio moja, alisema kuna Maprofesa wawili waliostaafu kutoka katika chuo kikuu cha Jerusalem walitembelea katika nyumba yetu ya Mbashiri kule Kababir na wageni wao wawili. Anasema, tulifanya mazungumzo nao na pia tuliwaonyesha mfumo wa jamaat wa kujitolea fedha. Mmoja ya wageni ambae alikuwa Profesa kutoka Austria mwishoni mwa mazungumzo alisema kitu kimoja kikubwa ninachokipenda kuhusiana na Jamaat Ahmadiyya ni juu ya mfumo wa utoaji wa fedha. Na alisema zaidi, shabaha yenu ni kuleta mageuzi ya upatikanaji wa utajiri halali, nawapongeza katika hilo.

Huzur(atba) alisema katika utoaji wa michango mali ya halali ni jambo la lazima. Mungu Mwenyezi alisema toeni katika kile kilicho halali, kile kilichopatikana kwa haki na sio kilichopatikana kwa njia za haramu. Sio ulichookoa katika kodi, au sio kilichopatikana katika njia nyingine zisizo halali. Hivyo michango ya jamaat inapokelewa kwa wale tu ambao wanapata vipato vya halali au angalau ijulikane ya kwamba wanapata vipato katika njia zisizo za haramu. Na ikiwa mtu anapata fedha katika njia zisizo za halali basi nidham ya Jamaat isikubali kupokea kipato chake.

Na ikiwa kwa kujua kabisa mchango huo ukachukuliwa basi aidha mchango wake utarudishwa au viongozi wataondolewa katika nafasi zao. Hivyo cha msingi ni kwamba, toeni mali zilizo halali. Hivi ndivyo baraka zitakavyopatikana. Wasiokuwa Waahmadiyya wanakubali jambo hili kama vile yule Profesa alivyokubali. Jambo hili linakuwa ushahidi kwa watu wa kidunia kuwa watu hawa ndio watakaoleta mapinduzi. Kwa kadiri lengo letu litakavyo bakia kuwa zuri, na kwa kadiri tutakavyoendelea kutafuta vilivyo halali na kutoa hivyo katika njia Mungu Mwenyezi, hapo ndipo tutakapoweza kuleta mageuzi. Na mageuzi hayo ndio shabaha yetu. Kwa sababu ni ahadi ya Mungu Mwenyezi pamoja na Masih Aliyeahidiwa(a.s), hatuna haja ya kuleta mageuzi yoyote ya kidunia bali tunaleta mabadiliko ya kiroho. Tunatakiwa kusambaza ujumbe wa Mtume Muhammad(s.a.w) duniani kote. Kusimamisha umoja wa Mwenyezi Mungu na kutimiza haki za viumbe wake. Na hii sio kauli mbiu ya kidunia. Bali Mungu Mwenyezi amemuahidi Masih Aliyeahiiwa(a.s) kusimamisha kundi la watu wenye moyo safi na wanyenyekevu ambao watakamilisha kazi hii. Ambao watajitolea kila kitu kukamilisha kazi hii.

Huzur(atba) alisema Masih Aliyeahidiwa(a.s) akizungumzia juu ya imani ya Jamaat yake alieleza mifano iliyoonyeshwa na Masahaba wa Mtume(s.a.w) ya imani na unyenyekevu ambayo ilikuwa tofauti kabisa na dunia hii. Walichukulia kila shida kuwa ni jambo la kawaida kwao, kiasi hiki ya kwamba walihama nchi zao walizozipenda, walijitenga na mali zao, familia zao na rafiki zao. Hivi ndivyo niionyavyo Jamaat yangu waonyeshe kiwango cha shauku kubwa kwa Mungu Mwenyezi na pia waonyeshe ile rangi halisi ya unyenyekeu na Imani, Huzur(atba) alisema, Masih aliyeahidiwa(a.s) alisema: Kuhusiana na kujitolea fedha, kwa ajili ya lengo na dhumuni la dini wanajamaat wangu wanatoa michango kwa moyo mkunjufu. Akasema zaidi kila mmoja anatimiza wajibu huu sawa na uwezo wake. Ni Mwenyezi Mungu pekee ndiye ajuae ni kwa nia gani na imani gani mtu anashiriki katika utoaji wa michango.

Alisema ninajua vizuri kabisa kwamba Jamaat yangu inaonyesha ile imani na uamanifu ambao Masahaba wa Mtukufu Muhammad(s.a.w) waliuonyesha katika kipindi kigumu.

Huzur(atba) alisema wakati fulani Masih Aliyeahidiwa(a.s) kwa kuona kiwango cha kujitolea cha Masahaba zake alielezea namna gani walivyokuwa wanajitolea. Huzur(atba) alisema, hivyo Masih Aliyeahidiwa(a.s) alipandikiza aina ile ya mapinduzi kwa Masahaba zake ambayo iliwafanya watupilie nyuma ya migongo yao tamaa za vitu vya kidunia na kuipa dini kipaumbele. Lakini hali ya kiroho aliyoipandikiza kwa Maswahaba zake haswa wale masahaba waliojiunga moja kwa moja kwa mkono wake, je hali hiyo ilikufa, au hali hiyo iliishia hapo, au hali ile ilikuwa kwa kipindi kile tu, ikiwa kama ni kweli na ikiwa kama ingefanyika kwa kipindi kile tu basi kusingekuwa na maendeleo yoyote ya Jamaat.

Mungu Mwenyezi alimuahidi kwamba atajulikana kila pembe ya dunia tena kwa heshima. Kuwapata wenye uaminifu na watakaojitolea, kulihitajika katika Jamaat. Vilevile baada ya kupata hizi habari njema kutoka kwa Mungu Mwenyezi alifikisha habari njema hizi katika Jamaat kuwa baada yake mfumo wa Ukhalifa utaanzishwa ambao utakamilisha kazi yake baada yake na kupitia huo wale wanajumuiya watiifu wa Jamaat watakamilisha kazi hii. Hivyo, leo tunaona jinsi gani Mungu Mwenyezi alivyoweza kutimiza ahadi yake. Kuna jamaat, ambayo ina watu watiifu sana walioshikamana na ukhalifa na wanajitolea maisha yao, mali zao na heshima zao. Huzur(atba) alisema na katika kutangaza mwaka mpya wa Tahrik Jadid nitataja baadhi ya matukio ya kujitolea ambayo yanahusiana na utoaji wa fedha. Huzur(atba) alisema kuwa matukio haya sio kutoka katika nchi tajiri bali ni kutoka katika nchi maskini kabisa na za wanajumuiya wapya. Ni jambo la kushangaza jinsi Allah alivyoibadili mioyo yao. Ijapokuwa ni maskini sana lakini ni jinsi gani wanavyojitahidi katika kujitolea.

Huzur(atba) alisema mmoja kati ya Wabashiri aliandika kuna Imam ambae alijiunga na Jamaat pamoja na msikiti wake. Alipoelezwa juu ya mfumo mzima wa jamaat wa kujitolea mali na Tahrik Jadid alisema kuwa yeye mwenyewe alikuwa anawafundisha watu namna ya kutoa michango na Zaka. Lakini hajawahi kuona mfumo madhubuti wa kujitolea kama huu katika sehemu nyingine yoyote wala hajapata kusikia. Kisha akatoa mchango wake na akaahidi kila mwezi sio tu yeye bali jamaat yote watalipa mchango wao kwa kudumu.

Huzur(atba) alisema kuwa watu hawa ni masikini wa hali ya chini kabisa lakini kwa kujitolea wapo juu sana. Hii sio habari ya nchi moja Huzur(atba) alisema, bali wimbi hili linavuma katika nchi nyingi za dunia.

Huzur(atba) alisema Mbashiri wa Ivory Coast aliandika siku moja walienda kwenye Tabligh katika kijiji fulani ambapo walifikisha ujumbe wa Jamaat. Watu wote wanaume kwa wanawake walisikiliza kwa makini. Mmoja wao alisema mara kadhaa kabla watu walishawahi kuja katika Tabligh, lakini hatujawahi kusikia ujumbe mzuri kama huu.

Kisha watu 300 walijiunga na jamaat Ahmadiyya. Baada ya hapo wakaelekezwa utaratibu wa kujitolea mali na mifumo mingine ya Jamaat. Lakini wakati wa mazungumzo waliambiwa kuwa leo ni siku ya mwisho ya Tahrik Jadid. Baada ya kujua hivyo Chifu na Imamu wa msikiti walisema ijapokuwa tumeipokea Ahmadiyya leo, lakini kwa njia yoyote

Endelea uk. 4

Tanzania yaingia kumi bora Afrika

Kutoka uk. 3

tutashiriki katika mpango huu wenye baraka. Kisha, watu wa kijiji hicho kwa haraka sana walikusanya kiasi cha Franga 10,000 na walilipa kama Tahrik Jadid.

Huzur(atba) alitaja tukio lingine kutoka Tanzania. Kuna mwanajamaat ambae ahadi yake ilikuwa laki mbili (200,000). Tayari alishalipa laki moja na ilikuwa bado anadaiwa laki moja aweze kuilipa. Walisema mwezi wa kumi alikumbushwa kuwa alikuwa na shilingi laki moja bado anadaiwa na mwaka wa Tahrik Jadid unaisha. Alisema alikuwa kwenye safari lakini alisema ataanda mipango ya kutuma fedha. Hivyo alituma fedha yake kupitia dereva wa basi.

Alimwambia dereva kuwa huu ni mchango wangu na unatakiwa kufika leo. Hivyo, atakapofika tu akabidhi fedha hizo kwa Mbashiri. Akampatia jina na namba za mawasiliano za Mbashiri. Hivyo dereva alipofika kituo cha Mabasi alimpigia simu Mbashiri na kumwambia ana hela zake hivyo anaweza kuja kuchukua. Mbashiri alipokuja kuchukua dereva akasema yeye pia anahitaji kuwa Ahmadiyya.

Huzur(atba) alisema watoto na mke wa dereva wa basi hilo tayari wameshakuwa Waahmadiyya, asingeweza kujiunga kama hakuridhika na jamaat. Dereva alimueleza mbashiri kuwa nilikuwa natembea huku nikiwa nina mawazo ya tukio hili kuwa katika dunia hii ya kupenda mali, ambapo binaadamu anapeda sana mali na pia sisi tupo katika nchi masikini. Je ni jinsi gani Mungu Mwenyezi amewafanya watu hawa waweze kutoa katika njia yake na kupata utulivu wa kweli. Huzur(atba) alisema hivi ndivyo kutuma mchango wa Ahmadiyya kulivyo kuwa chanzo cha asiyekuwa Ahmadiyya kujiunga na Ahmadiyya. Hivyo kuna michango inayotolewa kwa moyo safi ambayo inatoa majibu ya haraka.

Kujitolea fedha ambapo kulitokea kwa aliyetoa mali yake kwa mapenzi ikawa sababu ya kumuongoza mwenye roho safi. Hivi ndivyo Mungu Mwenyezi anavyotumia vyazo tofauti kulipa kwa matunda yake.

Huzuur (atba) alisema kwamba hali kadhalika Amir Sahib wa Senegali ameandika kwamba mwanjumuiya wao mmoja baba wa Omar Sahib ambaye hakuwa mwanajamaat alikuja kutokea mji mwingine akiwa na maradhi makali. Baada ya uchunguzi wa kina madaktari walishauri afanyiwe upasuaji wa tezi dume. Lakini Omar Sahib alikuwa hana fedha za kutosha kwa ajili ya upasuaji huo. Na ilikuwa vigumu pia kuchukua mkopo mkubwa kiasi hicho. Alipatwa na mashaka sana. Amir Sahib ameandika kwamba kwenye wiki ya kwanza ya Oktoba wakati wa hotuba ya Ijumaa aliwakumbusha Wanajumuiya, kesho yake Omar Sahib alikuja na aliomba akatiwe risiti kwa mchango wake. Kwa kuwa Amir Sahib alikuwa anajua hali yake ya kifedha, alimwambia kwamba baba yake ni mgonjwa na anahitaji fedha kwa ajili ya matibabu yake katika hali kama hiyo anawezaje kujitolea namna hiyo. Omar Sahib alisema kwamba, jana kwenye hotuba ulisema kwamba hii ni biashara na Mungu Mwenyezi na nimekuja kufanya biashara hiyo na Mungu Mwenyezi. Hivyo nikatie risiti yangu..

Amir Sahib ameendelea zaidi kuandika kwamba siku mbili baadae alipokwenda nyumbani kwa Omar Sahib kumuangalia baba yake. Baba yake alikuwa amekaa kwenye kiti nje ya nyumba. Baadae Omar sahib alikuja na akasema kwamba biashara yangu na Mungu Mwenyezi imekuwa ya manufaa kwa sababu baba yangu hakupata maumivu yoyote na anajisikia vizuri. Baada siku mbili walipompeleka kwa daktari kwa ajili ya vipimo daktari alisema kwamba sasa upasuaji hauhitajiki. Baada ya tukio hili baba yake pia alijiunga na Ahmadiyyat.

Huzuur (atba) alisema kwamba haya ni malipo ya dhahiri ambayo Mungu Mwenyezi huwa Anayafanya wakati fulani fulani. Alisema kwamba wiki ilioyopita wakati wa uzinduzi wa msikiti alielezea tukio la mtu mmoja ambaye alijiwekea kipaumbele cha kuhudumia msikiti na Mungu Mwenyezi Alimjaalia kiasi kikubwa cha fedha. Mtu wa kidunia ataliona hili kuwa ni bahati tu lakini muaminio anaamini kwamba kwa hakika ilikuwa ni Baraka ya Mungu Mwenyezi.

Huzuur (atba) alisema kwamba halikadhalika kuna Jamaat huko Congo, Kinshasa. Ayub Sahib mwanajumuiya anasema kwamba hapo kabla alikuwa hashiriki katika kazi zozote za Jamaat. Anasema mtoto wake wa kiume daima alikuwa mgonjwa mgonjwa na fedha nyingi zilitumika katika matibabu yake. Anasema kwamba alipopewa jukumu la kuwa Katibu wa Fedha aliwaza kwamba kujitolea kwake kifedha kuwe ni mfano kwa Jamaat. Huzuur (atba) alisema kwamba kwenye sehemu ya mbali na ndogo ya dunia mtu anapopewa jukumu la Katibu wa Fedha, kujitolea kwake kifedha kunakuwa ni mfano. Alisema zaidi kwamba alianza kuwa anatoa michango yake kwa kufuata viwango na kwa baraka za hilo hali yake ya kifedha ikaanza kuboreka. Maisha yakaanza kuwa tulivu na yenye raha. Hivi sasa mtoto wake pia yuko salama na magonjwa. Anasema kwamba anaona kuwa yote hayo ni kutokana na huduma kwa Jamaat na kujitolea kimichango.

Huzuur (atba) alisema kwamba sisi sote tumewahi kusikia msemo huu; "Jitolee kwa kukata tumbo lako", lakini ni vigumu kufikia kina chake na maana yake isipokuwa tu upatapo uzoefu. Lakini kwa kuangalia masikini wajitoleavyo inakuwa ni rahisi kuelewa maana zake. Huzuur (atba) alisema kwamba mwanamke mmoja kutoka Gambia alijiunga na Ahmadiyya na alipoambiwa kuhusu Tahrik-i-Jadid alisema kwamba ana dalasi mia moja tu kwa ajili ya kununulia mchele na alikuwa hana mchele wowote. Alisema zaidi kwamba mtoto wake pekee wa kiume aliye naye ametoweka kwa miaka miwili iliyopita na watu wanasema kwamba huenda amesha kufa kwa kuwa kwa miaka miwili iliyopita kumekuwa hakuna habari yake yoyote. Kwa hiyo alizitoa hela zile kwa ajili ya Tahrik-i- Jaded na akasema kwamba Mungu Mwenyezi Atamtengenezea. Siku tatu baada ya tukio hili mtoto wake alirudi na akamletea mifuko kumi ya mchele na kiasi kikubwa cha fedha. Alimueleza kuwa wakati alipokuwa hapatikani alikuwa anajifunza kazi za ujenzi na sasa anapata tenda kubwa za ujenzi katika mji huo. Kutokana na hilo yeye mwenyewe anasema kwamba ni kutokana na kujitolea kwangu na kuanzia sasa daima nitafanya hivyo.

Huzuur (atba) alisema kwamba je haya si mapinduzi kwamba kwa kumpokea Masihi Aliyeahidwa (AS), Mungu Mwenyezi Ameyaweka kwa watu wenye kuishi sehemu za mbali namna hiyo. Huzuur (atba) alisema kwamba bila shaka ni hivyo. Alisema muangalieni mwanamke huyu ni juu kiasi gani imani yake imefikia. Hakujali njaa yake na Mungu Mwenyezi Amembariki kwa fadhila Zake.

Huzuur (atba) alisema kwamba kutoka Mali Mbashiri wetu anaandika kwamba mwanamke ambaye ana umri wa miaka themanini na anatoa michango yake kwa viwango; siku moja alikuja akitembea kutokea kilometa moja kwenye jua kali kutoa mchango wake. Mbashiri alisema kwamba angekuja kuuchukua lakini alisema kwa kuwa amesikia umuhimu wa kujitolea kifedha hakutaka kupoteza baraka zake, hivyo aliona kwamba aje mwenyewe na kuufikisha mchango huo. Alitembea kuelekea nyumbani kwa Mbashiri kukiwa na jua kali ili kuokoa nauli na akajumlisha hela hizo kwenye mchango wake. Huzuur (atba) alisema kwamba hii ndio hadhi ya watu wanaoishi sehemu za mbali. Alisema kwamba jinsi Mungu Mwenyezi Anavyoimarisha imani za wanajumuiya kwa uzoefu binafsi ni bayana katika kila tukio.

Huzuur (atba) alisema kwamba Mbashiri kutoka Benin, Zakaria Sahib, anasimulia tukio na anasema kwamba Raisi wa moja kati ya matawi ya huko alipoteza kazi yake na alipatwa na mashaka. Katika siku hizo alikumbushwa kuhusu Tahrik-i- Jadid. Baada ya siku chache alikuja na akasema kwamba alipokumbushwa kuhusu Tahrik Jadid alipatwa na wasiwasi sana na alimuomba Mungu Mwenyezi Ampatie chanzo fulani ili aweze kulipa mchango huo. Anasema kwamba alipitisha usiku akiwa na mateso sana. Asubuhi alipokwisha sali Fajr alikwenda kwenye kijiji cha jirani kutafuta kazi. Anasema kwamba hakupata kazi yoyote pale lakini kulikuwa na mtu ambaye alikuwa akienda sokoni kwa ajili ya kuuza wanyama wake. Anasema kwamba alimsaidia na kwa shukurani alimpa Franga 500. Kutoka na hizo alitumia Franga 200 kwa ajili ya chakula na akampa Franga 100 mtoto wake aliyekuwa anakwenda shule na Franga 200 zilizobaki akalipa mchango wake wa Tahrik-i-Jadid. Anasema kwamba kutokana na kulipa mchango Mungu Mwenyezi Amembariki na baada ya siku nne hasa akapata kazi. Anasema kwamba haiwezikani kuwa ni bahati tu hiyo, lazima ni baraka ya Mungu Mwenyezi.

Huzuur (atba) alisema kwamba baada ya Afrika kuna matukio huko India pia. Inspekta wao Shahabuddin Sahib ambaye ni inspekta wa Tahrik-i-Jadid wa Talangana na Andhra anaandika kwamba rafiki mmoja kutoka Hyderabad ambaye anatokana na familia ya kimasikini alianzisha biashara kwa Rupia 20,000. Ana duka dogo. Wakati wa sala anafunga duka lake. Huzuur (atba) alisema kwamba hii ndiyo adhama ya muaminio. Anatoa pato zima la mwezi mmoja kwa ajili ya mchango wa Tahrik-i-Jadid. Mwaka huu alilipa rupia 60,000 kwa ajili ya Tahrik-i-Jadid. Anaishi kwenye nyumba ya kupanga. Inspekta sahib anasema kwamba siku moja alimuuliza kwa nini hanunui nyumba yake mwenyewe. Alijibu kwamba ache iwe kama ilivyo kwa sababu dunia hii hata hivyo inaelekea kwenye kuangamia. Hivyo kwa nini nikusanye fedha, ni vyema niitumie katika njia ya Mungu Mwenyezi.

Huzuur (atba) alisema kwamba hali kadhalika kutoka Pakistani Naibu Wakil Maal anaandika kwamba alikutana na Khadim kutoka Sialkot ambaye aliahidi Rupia 20,000. Anasema kwamba alimuambia aongeze hadi rupia 100,000 naye akakubali. Alianzisha biashara ya kusafirisha nje alikuwa akilipa Rupia 5,000 na kisha Rupia 10,000 na kisha Rupia 15,000 na kisha akaongeza kufikia Rupia 100,000. Alisema kwamba ni kutokana na Baraka za michango kwamba amekinunua kile kiwanda alichokuwa amepanga.

Huzuur (atba) alisema kwamba halikadhalika kutoka Indonesia Mbashiri ameandika kwamba kulikuwa na mtu aliyesema kwamba kama akipata pikipiki itakuwa rahisi kwake kuhudhuria sala za ijumaa pamoja na mtoto wake wa kiume. Huzuur (atba) alisema kwamba Mbashiri wetu alimwambia kufanya maombi na atoe michango kwa viwango. Mbashiri sahib anasema kwamba alilipa michango yake na ya familia yake kwa viwango. Baada ya siku chache Mungu Mwenyezi Alimbariki na aliweza kununua pikipiki. Pato lao la nyumbani liliongezwa na amefanya Wasia pia na sasa ana pikipiki tatu nyumbani kwake.

Huzuur (atba) alisema kwamba hapa Canada pia kuna watu ambao wanaongeza michango yao. Mtu mmoja aliongeza mchango wake kutoka dola 1,000 hadi dola 5,000 na ili kuvuna Baraka za Mungu Mwenyezi alilipa hiyo mwanzoni. Alilipa dola 20,000 kwa ajili ya ujenzi wa msikiti pia.

Huzuur (atba) alisema kwamba hali kadhalika kuna matukio hapa pia yenye kuchangamsha imani. Kulikuwa na mwanamke mmoja aliyeahidi dola 1,000. Lakini hakuwa na fedha. Jioni mumewe alimwita na kumwambia kwamba mtu yule na yule wamempa cheki. Hapo akamuuliza ni ya dola 1,000? Akajibu ndiyo, lakini alijuaje, aliuliza. Alijibu kwamba alikwa na wasiwasi wa kulipa dola 1,000 kwa ajili ya Tahrik-i-Jadid. Hivyo aliona kwamba ni lazima iwe ni mpango wa Mungu Mwenyezi hivyo lazima iwe ni kiasi hicho hicho.

Huzuur (atba) alisema kwamba hali kadhalika kuna nchi za Ulaya, jumuiya mpya zinaanzishwa huko. Mbashiri wa Micronesia anaandika kwamba kutokana na umasikini wa kule kuna uhaba wa kazi. Kuna idadi kubwa ya watu ambao hawana chanzo chochote cha mapato. Aidha wanawategemea ndugu zao kupata fedha kiasi kutoka kwao au kibarua cha siku moja au mbili ambazo kwazo wanaishi. Miongoni mwao yumo mzee mmoja ambaye anapenda kufanya kazi za Jamaat na anatumia takriban muda wake wote kufanya kazi za Jamaat. Hata kama hakuna kazi za Jamaat anajaribu kufanya kitu fulani kitakacho faidisha Jamaat. Kwa mwaka mmoja uliopita alikuwa anaokota

Endelea uk. 5

Tanzania yaingia kumi bora Afrika

Kutoka uk. 4

makopo matupu kuyauza kama mali ghafi. Mwaka mzima alikuwa anaokota makopo na kisha anayauza kama mali ghafi kwa dola 30. Kisha anakwenda msikitini na kulipa dola 10 kwa ajili ya mchango wake wa Tahrik-i-Jadid. Katika mwaka huo chochote alichopata alitoa theluthi yake kwa Jamaat.

Huzuur (atba) alisema kwamba kutoka Ujerumani Katibu wa Tahrik-i-Jadid ameandika kwamba kuna mwanamke ambaye hakutaka jina lake litajwe alikuja kwenye ofisi ya Tahrik-i-Jadid na akatoa vito vyake vyote. Vilikuwa vingi kiasi hiki kwamba meza yote ilijaa vito hivyo. Kulikuwa na mikufu, bangili za dhahabu, pete, na aina nyingi nyingine za vito. Lakini alisema jina lake lisitajwe ili kujitolea kwake kubaki kuwa ni kwa ajili ya Mungu Mwenyezi. Huzuur (atba) alisema kwamba wanawake wanapenda vito lakini ni wanawake wa Kiahmadiyya wanaofanya dhabihu hizi. Hapa mwanamke mmoja Muahmadiyya alionana nami ambaye aliniambia kwamba alitoa vito vyake vyote. Lakini ndugu za mume wake hawakulipenda hilo hivyo walimsimanga na kumlaumu. Huzuur (atba) alisema kwamba Mungu Mwenyezi Anawabariki wale wanaojitolea katika njia Yake na bila shaka Atambariki mwanamke huyu pia. Lakini wale watu lazima wawe na wasiwasi wanaowazuia wengine wasijitolee kifedha. Ni Mungu Anayetoa mali na ni Yeye Anayeweza kuichukua tena kutoka kwa asiye na shukurani - daima lazima ikumbukwe. Hivyo wale ambao mioyo yao inapata fikra za aina hiyo watubu na waombe msamaha sana.

Huzuur (atba) alisema kwamba kuna matukio mengi huko Urusi pia. Rafiki mmoja alisema kwamba alikuwa masikini sana. Alikuwa akiishi kwenye nyumba ya kupanga na alizungukwa na matatizo mengi ya kifedha. Lakini alikuwa akilipa michango yake ya lazima na Tahrik-i-Jadid sawa na uwezo wake. Alisema kwamba kutokana na baraka za michango mke wake alipata kazi serikalini mara tu alipomaliza Chuo cha Udaktari. Na Serikali ikawapa mkopo kwa ajili ya nyumba kwa watoto. Na sasa wana gari mbili pia. Anasema kwamba yote hayo ni kutokana na baraka za michango. Mwanzoni tulikuwa tukilipa michango katika hali ngumu lakini sasa tuna afueni.

Huzuur (atba) alisema kwamba Mungu Mwenyezi Anawabariki watu huko Urusi, Afrika, Indonesia na nchi zingine pia na Ulaya pia. Baraka zote hizi za Mungu Mwenyezi ni ushahidi wa kile Alichomuahidi Masihi Aliyeahidiwa (AS) kwamba Atampatia kundi la waaminio na Atawazidisha katika imani pia. Wale watu wanaotembea kuelekea kwa Mungu Mwenyezi Anawaongeza kiimani pia.

Huzuur (atba) alisema kwamba anayo matukio mengi ya kujitolea kifedha na ilikuwa vigumu kwake kuchagua yepi ayachukue na yepi asiyachukue. Kwa vyovyote, akasema, nimewaelezeni machache tu kati yao. Huzuur (atba) alisema kwamba katika nchi zote kuna hali hiyo hiyo ya Mungu Mwenyezi. Wale wanaomtegemea Mungu Mwenyezi Amewabariki kwa wingi. Kwa mtu yeyote mwenye akili timamu huu ni uthibitisho tosha wa ukweli wa Ahmadiyya kwamba ni jinsi gani Mungu Mwenyezi Anawabariki wale wanaojitolea katika njia yake.

Huzuur (atba) alisema kwamba ni kwa sababu michango hii inatumika katika kueneza dini Ya Mungu Mwenyezi. Watu kutoka nchi masikini bila shaka wanatoa michango lakini matumizi yao ni makubwa sana kulinganisha na michango yao. Hii ndio sababu makao makuu inatumia michango inayotolewa na nchi tajiri kutumika katika zile nchi maskini ambazo bajeti zao hazifikii mahitaji yao. Mamia ya shule, dazeni za mahospitali, mamia ya nyumba za wabashiri, mamia ya misikiti inajengwa kila mwaka na fedha zinahitajika kwa ajili ya hayo, ambazo zinatolewa katika mifuko ya Tahrik-i-Jadid na Waqf-i-Jadid. Hali kadhalika mamilioni ya dola zinatumika kwa ajili ya MTA. Ingawa pia kuna akaunti ya michango ya MTA na watu wanalipia hiyo pia, lakini matumizi ni makubwa zaidi.

Huzuur (atba) alisema kwamba kuhusiana na MTA ninataka kusema hili kwamba kutokana na utafiti, utazamaji wa MTA hauko kwa kiwango kile kinachopaswa. Au tunaweza kusema wanajumuiya hawasikilizi hotuba zangu za Ijumaa moja kwa moja (Laivu). Jumuiya inatumia kiasi kikubwa kwa ajili hiyo kwa mafunzo ya wanajumuiya. Kama kuna tofauti ya saa basi rudio la hotuba litizamwe. Wasio Waahmadiyya wengi wanaisikiliza na kisha wananiandikia kwamba wao sio waahmadiyya lakini wanasikiliza hotuba. MTA imefanywa kuwa ni njia ya kuiunganisha Jumuiya na Ukhalifa. Kama nyumbani kwako hutaweka umakini kuhusiana na hili basi taratibu watoto wako watapeperukia mbali. Mungu Mwenyezi bila shaka Atatimiza Ahadi yake aliyompa Masihi Aliyeahidiwa (AS), InshaAllah - watu waaminifu watajiunga pia.

Huzuur (atba) alisema kwamba mmeona kilele cha uaminifu kwa wanajumuiya wapya. Isije, ikatokea kwamba wanajumuiya wapya wanapata baraka zote na wa zamani wakajibanza katika sifa kwamba baba na babu zao walikuwa ni Masahaba wa Masihi Aliyahidiwa (AS) na kwamba wao ndio wanajumuiya wa mwanzo. Mungu Mwenyezi Hana uhusiano wowote binafsi na yeyote. Kama wanajumuiya wa zamani wanajiweka mbali basi haitajalisha kwamba baba zao na babu zao walikuwa ni Masahaba wa Masihi Aliyeahidiwa (AS). Hivyo, kabla ya hili tubuni kwamba mjigandishe kwenye Ukhalifa. Na kwa hilo njia nzuri kuliko zote ambazo Mungu Ameianzisha ni MTA- itumieni. Kuna vipindi vingi vingine kwenye MTA lakini angalau msikilize hotuba. Sio kwamba Mbashiri amesoma muhtasari na hivyo sasa mnajua kilichosemwa kwenye hotuba. Kuna tofauti kubwa kati ya kusikiliza muhtasari na kusikiliza hotuba nzima.

Huzuur (atba) alisema kwamba kama alivyokwisha sema hapo kabla mwaka wa Tahrik-i-Jadid umeisha na mwaka mpya umeanza. Na sasa ninatangaza mwaka mpya wa Tahrik –i-Jadid. Amesema kwamba anafikiri kuwa ni kwa mara ya kwanza kwamba mwaka mpya wa Tahrik-i-Jadid unatangazwa kutokea Canada. Ni baraka za Mungu Mwenyezi kwamba Jamaat imepanuka sana kiasi hicho. Mwaka 1934 Ahrar walizungumzia kuimaliza Jamaat, na kuigeuza Qadian kuwa kifusi. Katika wakati huo Hadhrat Musleh Mauud (RA) alitangaza mpango wa Tahrik-i-Jadid na alipanga kupeleka Wabashiri duniani kote. Mpango thabiti wa kueneza Islam uliwekwa. Na leo kwa baraka za Mungu Mwenyezi Jumuiya inajulikana duniani kote. Jamaat imeanzishwa katika nchi 209 duniani. Leo hii jua halizami kwenye Jumuiya. Kulikuwa na wakati ambapo Ahrar walikuwa wakizungumzia kuifuta Jamaat huko Qadian na leo kutoka kwenye kona nyingine ya dunia mtumishi wa Masihi Aliyeahidiwa (AS) anapeleka ujumbe wake duniani kote. Ahadi ambayo Mungu Mwenyezi Aliitoa kwa Masihi Aliyeahidiwa (AS) inatimizwa kwa heshima kubwa. Hivyo ikimbukwe na kila Muahmadiyya kwamba mambo haya yanaweka majukumu kwa kila mmoja wao. Na kutimiza majukumu haya ni wajibu wa kila mmoja wenu.

Huzuur (atba) alisema kwamba sasa ninatangaza mwaka mpya wa Tahrik-i-Jadid. Kwa Baraka za Mungu Mwenyezi mwaka ulioishia Oktoba 31 ulikuwa wa 82 na kuanzia tarehe moja Novemba mwaka wa 83 tayari umeisha anza.

Huzuur (atba) alisema kwamba kwa Baraka za Mungu Mwenyezi taarifa zilizopokelewa kutokana na hizo katika mwaka uliopita Jumuiya ya Ahmadiyya imepata fursa ya kufanya dhabihu ya Paund za Kiingereza 1,933,000.00. Shukurani zote zinamthibitikia Allah. Hii kwa kulinganisha na mwaka uliopita ni ongezeko la Paund 701,700.00

Huzuur (atba) alisema kwamba kinafasi Pakistani daima ni ya kwanza. Vinginevyo ya kwanza ni Ujerumani, ya pili ni Uingereza, ya tatu ni Amerika, ya nne ni Canada, ya tano ni India, ya sita ni Australia, ya saba ni nchi ya Mashariki ya kati, ya nane ni Indonesia, ya tisa ni nchi nyingine ya Mashariki ya kati, ya kumi ni Ghana, ya kumi na moja ni Switzerland. Alisema kwamba orodha ya nchi bora huishia kumi lakini kwa kuangalia malipo ya mtu mmojammoja ni ya juu sana huko Switzerland na hii ndio sababu jina lake limewekwa chini ya orodha ya nchi bora.

Huzuur (atba) alisema kwamba kwa kuangalia malipo ya mtu mmojammoja nambari ya kwanza ni USA, kisha Switzerland, Uingereza, Finland, Singapore, Ujerumani, Norway, Japan, na Canada. Lakini kabla ya hilo kuna Jamaat tano za Mashariki ya kati hatuzitaji majina yao. Katika Afrika kwa makusanyo ya jumla ya kwanza ni Mauritius, kisha Ghana, Nigeria, Gambia, Afrika Kusini, Burkina Faso, Kameruni, Sierra Leon, Liberia, Tanzania na Mali.

Huzuur (atba) alisema kwamba kuhusiana na idadi ya washiriki watu wapya 90,000 walishiriki na jumla ya washiriki ni 1,404,000. Jitihada bora kabisa za kuongeza washiriki zilifanywa na Benin, Niger, Mali, Burkina Faso, Ghana, Liberia, Senegal na Kameruni. Alisema kwamba hapo ndipo kila mmoja ashike nadhari duniani kote.

Huzuur (atba) alisema kwamba kwa baraka za Mungu Mwenyezi Daftar Awwal bado liko wazi na linaendelea na malipo yanakuja baadhi kwa vizazi vyao marehemu na baadhi kwa wale ambao bado wako hai. Huko Pakistan kuna Jamaat kubwa tatu. Kati ya hizo ya kwanza ni Lahore, pili ni Rabwah na ya tatu ni Karachi. Kisha kuhusiana na kujitolea miji kumi ya kwanza ni kama ifuatavyo: Islamabad, Multan, Quetta, Peshawar, Gujranwala, Hyderabad, HafizAbad, Mianwali, Kotli, Khanewal na Bahawalpur.

Huzuur (atba) alisema kwamba kuhusiana na kujitolea wilaya kumi bora huko Pakistani ni kama ifuatavyo: Alisema kwamba ingawa kuna umasikini kujitolea kwa Pakistan ni kwa hadhi ya juu. Sialkot, Faislabad, Sargodha, Gujrat, Omer Kot, Okara, Narowal, Mirpur Khas, Toba, Take Sing, Mandi Bahauddin, na Mirpur Azad Kashmir.

Huzur (atba) alitaja jamati kumi bora za Ujerumani na kisha mikoa kumi bora ya Ujerumani. Imarati kumi za ndani ya Ujerumani pia zilitangazwa.

Huzuur (atba) alitaja mikoa mitano bora ya Uingereza ambayo ni kama ifuatavyo: London B, London A, Midland, North East na South Region. Na Jamaat bora kumi ni Msikiti wa Fazl, Worcester Park, Glasgow, Birmingham South, New Malden, Bradford, Islamabad, Gillingham, North West na Wimbledon Park. Huzuur (atba) alisema kwamba kwa kuangalia malipo ya mtu mmojammoja mikoa mitano ya kwanza ni South West, Islamabad, Scotland, Midland, na North East. Na alitaja Jamaat kumi bora pia.

Huzuur (atba) alisema kwamba huko Canada Imarati bora ni Peace Village, Vaughn, Calgary, Brampton, Vancouver, Mississauga. Na kwa marejesho kumi bora za Canada ni: Edmonton West, Pelekadaram, Saskatoon South, Saskatoon North, Milton East, Ottawa West, Ottawa East na Regina. Huzuur (atba) alisema kwamba Jamaat ya Lloydminster haikupata nafasi yoyote wakati Raisi wa Jamaat hiyo anaonekana yu mwenye juhudi sana na hali ya kifedha kwa ujumla ya wanajumuiya ni nzuri pia.

Huzuur (atba) alisema kwamba kwa makusanyo ya jumla Jamaat ya kwanza huko USA ni Silcon Valley, kisha Oshkosh, Oshkosh two, Detroit, Seattle, York, central Virginia, Los Angeles, Silver Spring, Central Jersey, Chicago, Southwest, Los Angeles West.

Huzuur (atba) alisema kwamba Jamaat kumi bora za India ni Karallie, Karalla, Kalikat Karalla, Hyderabad, Andhra Pradesh, Patheprame Karalla, Qadian, Kenanoor Town, Karalla, Chingari Karalla, Delhi, Kolkata Bengal na Salore Tamal Nado. Huzuur (atba) alisema kwamba majimbo kumi bora ya India ni kama yafuatayo: Karalla, Kernatak, Andhra Pradesh,Tamil Nado, Jamu Kashmir, Uresa, Punjab, Bengal, Delhi na Maharashtra. Huzuur (atba) alisema kwamba katika miaka michache iliyopita India imekuwa bora sana waila walikuwa nyuma sana.

Huzuur (atba) alisema kwamba kwa Baraka za Mungu Mwenyezi pia wanakuwa bora. Jamaat kumi bora za Australia ni kama zifuatazo: Malbourne, Bervic, Castle Hill, ACT Canberra, Maestan Park, Brisbane, Longbazvick, Long Borne, Clapton, Melbourne East. Hali kadhalika Jamaat kumi bora kwa kuangalia ulipaji wa mmojammoja ni: Tasmania, Brisbane North, ACT Canberra, Sydney Metro, Darwin, Paramata, Melbourne, Bevic, Perth, Maestan park na Castle Hill.

Huzuur (atba) aliwaombea wanajumuiya waliojitolea katika Tahrik-i-Jadid kwamba Mungu Mwenyezi Abariki Mali zao na Apokee dhabihu zao na Awape fursa kushiriki katika kujitolea kwa wingi na waimarishe uhusiano wao na Ukhalifa, Amin.

Bustani ya Washairi

SAUTI KUTOKA MAKKA

1. Labaika Allah Labaika, Labaika Allah Labaika
Mola nimekuitika, Nyumba Yako nimefika
Nikipanda na kushuka, kwenye viunga vya Makka
Pekeyo Subhaanaka, Wahdahu laasharika.

2. Labaika Allah Labaika, Labaika Allah Labaika
Nipo paloamanika, Wahyi uliposhuka
Palosheheni fanaka, palindwa na Malaika
Ewe Chanzo cha baraka, Wahdahu laasharika.

3. Labaika Allah Labaika, Labaika Allah Labaika
Mbele yako naanguka, moyoni nimedhikika
Nalilia kusafika, nipate kutoharika,
Mola Ulotakasika, Wahdahu laasharika.

4. Labaika Allah Labaika, Labaika Allah Labaika
Mlangoni najiweka, ninajitoa sadaka,
Naomba kukubalika, ijapo nimedhofika
Mno Ulivyotukuka, Wahdahu laasharika.

5. Labaika Allah Labaika, Labaika Allah Labaika
Mbele yako natamka, nitayari kutumika
Vyote utavyoniweka, ni radhi nimeridhika.
Ewe Mwenye Mamlaka, Wahdahu laasharika.

6. Labaika Allah Labaika, Labaika Allah Labaika
Naomba kusameheka, ona nilivyochafuka
Wote nimeharibika, nimekuwa takataka.
Allah Jalla Jalaaluka, Wahdahu laasharika.

7. Labaika Allah Labaika, Labaika Allah Labaika
Naomba kumakinika, Mola ‘alaa dhikrika,
Na wingi wa shukurika, na wema wa ibadaka
Yaa Malikul Muluuka, Wahdahu laasharika.

8. Labaika Allah Labaika, Labaika Allah Labaika
Ninaomba kuongoka, njia iliyonyooka
Nishike sala na zaka, nyuma nisije geuka.
Iko juu Adhimuka, Wahdahu laasharika.

9. Labaika Allah Labaika, Labaika Allah Labaika
Nipe ninalolitaka, umbo jipya kuumbika
Kifo kilonigubika, Mola nipate huika
Ewe Mola Msifika, Wahdahu laasharika.

10. Labaika Allah Labaika, Labaika Allah Labaika
Unishushie baraka, kiangazi na masika
Nizidi kukukumbuka, daima bila kuchoka
Nyingi mno Fadhilika, Wahdahu laasharika.

11. Labaika Allah Labaika, Labaika Allah Labaika
Machozi yabubujika, kila ninapogeuka
Nyuso zitele wahaka, furaha imetoweka
Ewe uso dhalilika, Wahdahu laasharika.

12. Labaika Allah Labaika, Labaika Allah Labaika
Ewe usiye shindika, Swali alaa Rasulika,
Uma ulogawanyika, upate kuunganika
Ewe uso mshirika, Wahdahu laasharika.

OLE WAKO WE DUNIA

1. Nianze bismillahi, kwa jinale nafungua
Kumekucha asubuhi, niseme nawe dunia
Umepondeka wajihi, kwa moto wa nyukilia
Ole wako we dunia, umemkana Masihi.

2. Tokea hapo abadi, umejawa na kiburi
Zama za Nuhu na Hudi, ungali na ashirari
Huba yote ya wajudi, kwako imekuwa shari
Ole wako we dunia, umemkana Masihi.

3. Mbora wa manabia, kunena alimaliza
Kwa Allah nikirejea, mtaishi kwenye giza
Ila mahdi nabia, giza ataliondoza
Ole wako we dunia, umemkana Masihi

4. Umeshamiri majanga, nchi kavu na majini
Maradhi yasiokinga, ni yatele duniani
Kitali pia kimbunga, kadhalika na tufani
Ole wako we dunia, umemkana Masihi

5. Zimetoweka baraka, kila zao linakufa
Na kilimo cha masika, hakinacho tena sifa
Viumbe wahangaika, kila kona ni maafa
Ole wako we dunia, umemkana Masihi

6. Umefunga abuwabu, kwao wenye madaraka
Hawana tena sababu, kumuogopa rabuka
Hawana hata adabu, kwa watoto malaika
Ole wako we dunia, umemkana Masihi

7. Akili umezifunga, kwa wanao wa dunia
Eti mbali wajitenga, hawataki jumuia
Mashekhe nao waganga, wanyota kutabiria
Ole wako we dunia, umemkana Masihi

8. Dunia wanakupenda, hadi kupita kiasi
Penzi limekua inda, kila pembe adharusi
Waja nao wamekonda, wana wingi wasiwasi
Ole wako we dunia, umemkana Masihi

9. Dunia yetu ya leo, dini haina thamani
Waja hawana upeo, wamefeli mtihani
Kamari pia vileo, vyatangazwa mitaani
Ole wako we dunia, umemkana Masihi

10. Jicho unaliduaza, jinsi ulivyo mwerevu
Sayansi ukashangaza, ukajiona mpevu
Kwa Allah ukapooza, ukazidi upotevu
Ole wako we dunia, umemkana Masihi

11. Umezidi upuuzi, dunia umefumbata
Inapigiwa miruzi, michezo yenye utata
Hata kutaja siwezi, nafusi itanisuta
Ole wako we dunia, umemkana Masihi

12. Hata vyombo vya habari, dunia umezuia
Wayafumba ya kahari, ya masihi kuwadia
Na wengine kwa jeuri, ovyo kumtangazia
Ole wako we dunia, umemkana Masihi

13. Yote unayoyafanya, kitanzi umejivisha
Masihi angekuponya, ila sasa umekwisha
Nabii amekuonya, mara nyingi ukabisha
Ole wako we dunia, umemkana Masihi

14. Walombai Masihi, pia unawadhulumu
Kwa kufata usahihi, wawalipua mabomu
Wengi umewajeruhi, vifo na kumwaga damu
Ole wako we dunia, umemkana Masihi

15. Beti ya kumi na tano, hapa ninamalizia
Usipuuze maono, dunia na kuusia
Vita isiyo mfano, yatatu inakujia
Ole wako we dunia, umemkana Masihi

Mwl. Najat Fakim Said
NANG’OLO = THE BIG BOSS
KINEGEMBASI IRINGA.

KWA HAYO MATETEMEKO,
MOLA WETU TUNUSURU

1. Allahu Akbaru, twakiri Umoja wako
Tunakuomba Kaharu, Nusuru viumbe vyako
Tughofirie ghafaru, utukinge na matuko
Kwa hayo matetemeko, Mola wetu tunusuru.

2. Pole ndugu wa Bukoba, pole kwa matetemeko
Yaliyobomoa nyumba, mkakosa maegeko
Yakaleta na misiba, misiba mingi kuliko
Kwa hayo matetemeko, Mola wetu tunusuru.

3. Mola wetu tunusuru, kwa hayo matetemeko
Nusuru yasitudhuru, twakuomba waja wako
Tusitiri ya Sataru, twakuogopa kuliko
Kwa hayo matetemeko, Mola wetu tunusuru.

4. Au ndiyo zilzala, Amri kutoka kwako
Inafikia pahala, siri zote ni za kwako
Twakuomba lahaula, tunusuru waja wako
Kwa hayo matetemeko, Mola wetu tunusuru.

5. Twakuomba manusura, sisi ni wa hanga wako
Zielekeze sudura, tufate mitume wako
Tuombee masrura, mpendwa Khalifa wako
Kwa hayo matetemeko, Mola wetu tunusuru.

6. Likituka tetemeko, na yakija mafuriko
Hatusaki mazindiko, bali tunarudi kwako
Ili tuvushwe kivuko, kama Nuhu mja wako
Kwa hayo matetemeko, Mola wetu tunusuru.

7. Ingawa twatoa pole, kwa wahanga wa matuko
Napenda niwazindule, tuchungue maandiko
Tuyasome kwa upole, tufikiri si vicheko
Kwa hayo matetemeko, Mola wetu tunusuru.

8. Hivi huu mghafala, wa dunia na vituko
Watowe kao ghafula, tazama yao mafiko
Wamemsahau Mola, wakaacha maandiko
Kwa hayo matetemeko, Mola wetu tunusuru.

9. Mliotoa misaada, mie ninawapa heko
Kwa moyo uso na inda, wapokeao chereko
Mola awape faida, malipo yenu yaweko
Kwa hayo matetemeko, Mola wetu tunusuru.

Mwl. Mubarak Nyamihasi – Mwanza.

NDEGE

1. Salamu alaikumu, enyi mlo waungwana
Nina jambo la muhimu, kichwani lanitafuna
Niazimeni kalamu, niwajulishe watwana
Ndege sina pa salama, kosa langu miye nini?

2. Maisha yangu ya tabu, sina moja maskani
Mengi kwangu masaibu, muda wote mashakani
Nitashitaki kwa babu, aniweke rehemani
Kosa langu miye nini, ndege sina pa salama?

3. Nilifanya jitihada, kutafuta pa amani
Kaja dada wa ziada, kunifukuza shambani
Asema ameshapanda, n iondoke kwa mtini
Ndege sina pa salama, kosa langu miye nini?

4. Nikatafuta mkinga, nikaweka na kiota
Akaja na lake panga, anataka kuukata
Adai ameshapanga, wake mti kuukata
Ndege sina pa salama, kosa langu miye nini?

5. Nituliapo mtini, matunda kujivunia
Waja mbio wafitini, njia kujitafutia
Wakafika na sokoni, manati kuniundia
Ndege sina pa salama, kosa langu miye nini?

6. Sipendeki kwa machoni, nina ladha ulimini
Wanisifu midomoni, wakiri huko rohoni
Mola nipe pa amani, uniweke mapajani
Ndege sina pa salama, kosa langu miye nini?

7. Saba beti nimifika, namba iliyo matata
Machozi yanidondoka, zangu mbio zimekata
Kwa namba yake rabuka, lowengi twaitafuta
Ndege sina pa salama, kosa langu miye nini?

Al-Ustadhi Ally S. Magana – Dar es salaam
(The new big boss)

Sheikh Swalehe Mbaruku Kapilima Ametutoka

Na Mwandihi wetu, Dar es Salaam

Sheikh Swalehe Mbaruku Kapilima amefariki dunia usiku wa kuamkia Jumanne, tarehe 15/11/2016 saa sita na dakika kumi na mbili huko nyumbani kwake Duthumi, Morogoro baada ya kuugua kwa kipindi cha muda mrefu. *Innaa Lillaahi wa Innaa Ilayhi Raajiuun.*
Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima alizaliwa katika kijiji cha Njinjo, Kilwa, Mkoa wa Lindi mwaka 1916.
Alipata elimu ya msingi ya kujua kusoma na kaundika pamoja na elimu ya msingi ya dini ya kiislamu ikiwemo kusoma Quran na fiqhi na akafanya kazi ya ukarani kuanzia mwaka 1953.

Baadaye aliacha kazi hiyo ya ukarani na akaamua kufanya shughuli mbalimbali binafsi za kujitafutia maisha zikiwemo ufundi cherehani na uashi.

Alijiunga na Jamaat Ahmadiyya kwenye miaka ya mwanzoni mwa Jamaat kuhubiriwa hapa Dar es Salaam. Mara alipojiunga alitokea kuwa mhubiri mwenye mbinu za aina yake na jitihada na jazba kubwa kiasi kwamba kwa fadhili za Mwenyezi Mungu aliweza kupandikiza mafundisho ya Jamaat kwenye maeneo mengi na matawi kadhaa yalinzishwa kwa mkono wake hasa katika mikoa ya Pwani, Lindi na Morogoro.

Baada ya kujiunga na Jamaat Ahmadiyya Sheikh Swalehe Mbaruku Kapilima alikabiliwa na upinzani mkubwa hadi ikambidi kuhama kutoka kwao. Alipojiunga ndugu zake walikusanyika na wakafanya hila ya kumuua hata kwa sumu na waliposhindwa wakamwambia kwamba akifa hawatomzika. Ndugu hao ambao walikuwa wa rika lake walipata sabiini, lakini wote walifariki kabla yake na wengi wao, alikuwa akisema amewazika kwa mkono wake mwenyewe; naye Allah amempa umri mrefu wa karibu miaka mia. Amewacha mjane mmoja, watoto 11, wajukuu, 39 na vitukuu 28.

Sheikh Swalehe Mbaruku Kapilima alikuwa ni mtu anayependa kusoma na kuwafunza wengine kile akijuacho. Alikuwa amejikusanyia hazina kubwa ya vitabu mashuhuri vya Hadithi za Mtume s.a.w., vitabu vya lugha lugha ya Kiarabu, vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa a.s. na vile vya Jamaat kwa ujumla. Hata katika siku zake za uzee na ugonjwa alikuwa akiendesha darsa nyumbani kwake huku wahudhuriaji wengi wakiwa sio Waahmadiyya. Amewacha Wasia kwamba vitabu vyake vitumike kwa ajili ya matumizi ya Jamaat huko katika tawi la Duthumi.

Alikuwa ni mtu mwenye haiba ya aina yake, aliyependa kujenga urafiki na kuudumisha. Katika maisha yake alikuwa na marafiki wengi baadhi yao akiwaita wanangu na yeye wakimwita mzee wangu kiasi hiki kwamba kama usingeambiwa kwamba huyu ni mwana wa urafiki na huyu ni baba wa urafiki ingekuwa vigumu kung'amua. Hali hii aliendelea nayo hadi kufa kwake na hata baadhi ya waliohudhuria mazishi yake walikuwa ni watoto wake wa aina hiyo.

Alikuwa ni mtu mwenye moyo wa huruma na kuwasaidia wengine shida zao na aliishi kwa wema sana na majirani zake na watu wa kijijini kwake Duthumi. Watu wengi walihudhuria mazishi yake.

Al-Ustadhi Mhenga Khamisi S.S. Wamwera ambaye ni miongoni mwa wanafunzi wa Sheikh Swalehe Mbaruku Kapilima analengalenga machozi yake akiwa na haya ya kutuliwaza.

MASKINI JEMBE LETU!

Assalam alaykumu, ndugu zangu waadhama
Bila shaka mwafahamu, tukio la hili juma
Lile Jembe akramu, kotekote likivuma
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Swahihi khabari hizo, kama mlivyozipata
Bali hili sisitizo, kwamba kweli limepita
Jembe la miyaka mzo, miti lililokikata
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Jembe linalo khabari, kubwa sana za ajabu
Ndanimwe mu somo zuri, kujipatiya thawabu
Nitadokeza si siri, ili nasi tujaribu
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!



Sheikh Swalehe Mbaruku Kapilima

Jembe letu hili Jembe, lililosanwa kwa chuma
Ni kama jino la pembe, kwa fani ya taaluma
Tulisaniwa tutimbe, aridhi kwa kuilima
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Lili la chuma cha puwa, madhubuti na la maki
Ni kali lilivyokuwa, nyika zikitaharuki
Misitu kipanguliwa, huku lang'owa visiki
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Lilikichimbuwa ndago, nyasi zilizo korofi
Likiangusha magogo, miti ya myaka ulufi
Na mapori ya mipingo, ikawa kama misufi
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Jembe likikakatuwa, udongo wa mfinyanzi
Na mbegu zikifukiwa, na maji bila ajizi
Mavuno tumeambuwa, mazuri ya simulizi
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Mashamba yapo janibu, ya mbalimbali nchini
Karafuu, mizabibu, kahawa na zaituni
Aina tunahesabu, mazao huko kondeni
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Lilijulika kwa kazi, kwa kuwa lilithubutu
Ni kama vile kinyozi, mnyowa nywele za watu
Ni makini kwa palizi, halikusaza fukutu
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Lili Jembe maarufu, kote lilijulikana
Wengi sana wameshufu, likilima kwa namna
Ya uswafi na nadhifu, watu kilihibu sana
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Lilijizoleya swifa, kubwa zisizo kifani
Kwa shughuli ashirafa, zisokuwa aasani
Kupande wangu kaifa, jaje sipatwe huzuni?
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Ndiyo sisi wahusika, tumo kwa kiwango chetu
Haya yamedhihirika, kwenye mzunguko wetu
Wengi tumehamanika, kwani hili pengo kwetu
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Katika kilimo chetu, ndilo lililotumika
Upande wa huku kwetu, kiangazi na masika
Wanasikitika watu, leo hilo kuvunjika
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Mwenyewe nililimiwa, konde kubwa kwa hisani
Na mbegu nilipandiwa, nikausiwa "tunzani"
Kupaliya haachiwa, yatapoota majani
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Jembe limenichangia, nusu ya maisha yangu
Hapa nilipofikiya, mchango wake na wangu
Pema nimeibukiya, pamwe na kizazi changu
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Ni Jembe lilotumika, likiwa kama mtaji
Duthumi lafahamika, linajulika Ujiji
Njinjo watalikumbuka, na sana sana Rufiji
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Loo afanaaleki, Jembe sasa limeng'oka
Kilimo hakifanyiki, haliwezi shughulika
Twaduwaa halaiki, bali tunasikitika
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Nina huzuni moyoni, matozi tele matoni
Jembe limenihisani, mengi mno ya thamani
Kubwa kunifunza dini, namshukuru Manani
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Ya ilahi ya Jaliya, naliliya Jembe langu
Jembe nililoanziya, nalo kulima magugu
Leo metuvunjikiya, roho yahisi uchungu
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Kama kumepambazuka, mchana upatikane
Hilo limeshavunjika, Allah utupe lingine
Lilo imara mpaka, na hili lije lingane
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Tupe badala ilahi, tulime kama zamani
Tudamke asubuhi, tumeshika mkononi
Twende shamba tukawahi, ile ngwe ya jioni
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Qariu, Jembe si lile, si lile ulijuwalo
La ngwamba mpini ule, wa mti wa mjoholo
Jembe hili ni teule, Jembe hili silo hilo
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Hakika Jembe si Jembe, ni wetu twamliliya
Alo na swifa za Jembe, aliyeaga duniya
Awe pamwe na wajumbe, wema walotanguliya
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Mwalimu wangu wa kwanza, kwenye masomo ya dini
Alifu amenifunza, hadi kwenye Furukani
Kaniacha ninaweza, kuisoma kwa kughani
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Amefariki mzazi, mweledi wa mahubiri
Alitenda hii kazi, kwa haiba na kwa ari
Mola Mpaye makazi, ya pepo siyo ya nari
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Fakaifa aasaa, kwa ndugu yetu mpenzi
Ya Rabbi pepo fungua, umwingize abarizi
Mlaze kwenye takia, yaso chawa sisimizi
"KAA" limeshakatika, maskini Jembe letu!

Ya Allah Dhul Jalali, upokeaye maombi
Mjao mpe kivuli, pas o hari wala vumbi
Umuweke payaleli, apepewe kwa ulumbi
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Tunamuombeya Mungu, aliko sote ni kwetu
Bali nyororo na pingu, asivishwe baba yetu
Asikung'utwe virungu, astarehe janatu
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Uthamini kazi zake, alizozitenda hapa
Pandisha daraja lake, awe juu wa kuchupa
Mlipe malipo yake, asipatwe na kipapa
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Apokewe kwa sherehe, na malaika kirama
Pazuri astarehe, kwenye janatu naima
Nasi ijapo tarehe, twende huko kwa salama
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Shekhe Swaleh Kapilima, tunasema buriyani
Twakuombeya Karima, adhabu ya kaburini
Uwe kwa wenye heshima, wasiotiwa motoni
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Shekhe ulale salama, ulikofika nyumbani
Nasi twaja tuko nyuma, nisemavyo tu njiayani
Tunamuomba Rahima, Atufikishe peponi
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Japo kufa ni lazima, kila mja atakufa
Wanapoondoka wema, kama nyumba yenye ufa
Kuzibwa kwa hima hima, Atake Mola Latwifa
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Ewe Allah Mtukuka, Ndiye Wahidi Manani
Wa fadhila na baraka, na yeyote Hufanani
Walizi wanaondoka, atanililiya nani?
Maskini Jembe letu, "KAA" limeshakatika!

Historia ya Sheikh Swalehe Mbaruku Kapilima kwa urefu itachapishwa kwenye tolea lijalo. Inshallah.

Niliyojifunza Katika Ibada ya Hija

Hotuba iliyotolewa na Mwl. Abdulrahman M. Ame katika Jalsa Salana ya mwaka 2016.

Baada ya tashahud na suratul Faatiha, mzumgumzaji alisema: Neno Hajj maana yake hasa ni kutengeneza mahali kwa ajili ya kufanya ziara (al-qasd li-ziyarah), na katika istilahi ya Shari'ah ya Islamu, linamaanisha kutembelea Bait-Allah (Nyumba ya Allah) ili kutekeleza ibada ya faradhi. Bait-Allah ni miongoni mwa majina ambayo Ka'ba huitwa.

Kuhiji huko Kaaba ni nguzo ya Tano ya Islam. Hija inakusudiwa kuingiza ndani ya nyoyo za waaminio umuhimu wa nguvu ya pamoja katika lengo la kuwaunganisha wanadamu, katika kupamabana na tabia mbaya ya kuiangukia dunia na ladha zake na hatimae katika kufikia mapenzi ya kweli ya Allah.

Haya ndiyo malengo makuu ya Hijja.

Dhana hii ya kuhiji inaonekana takriban kwenye dini nyingi, lakini katika dini kadha sehemu za kuhiji zimesambaa huku na huko. Islam inao upekee katika hili kwamba kuna sehemu moja tu ya kufanya hija ambayo Ni Makka, ambapo waislamu, duniani kote, hutakiwa kukusanyika kwa ajili ya Allah tu. Mamilioni ya Waislamu kutoka mataifa mbalimbali, yenye rangi mbalimbali, lugha mbali mbali na tamaduni na makabila mbalimbali hukusanyika Makka mara moja kwa Makka kwenye ibada ya hija, tukio ambalo linakusudiwa kudhihirisha udugu wa kidunia kwa namna ambayo haiwezi kuonekana kwenye dini yoyote iwayo.

Kaaba kwa hakika ni nyumba iliyojengwa kale kabisa kwa ajili ya ibada ya Mungu mmoja, yumkini wakati wa zama za Adam Fulani na hata Nabii Ibrahim alikuja kuikuta ikiwa imebomoka na kuziinua tena kuta zake, kama aya ionyeshavyo:

Mola wetu, hakika mimi nimewakalisha baadhi ya wazao wangu katika bonde lisilozaa karibu na Nyumba Yako Takatifu (14:38).

Watu walianza ibada hii ya Hija tangu enzi za Nabii Ibrahim lakini baadae muanguko ukatokea na Ibada hii ikabaki kuwa ushirikina na ujahili mtupu. Inasemwa kwmba ilifikia mahala ikaamuliwa kwamba ni Makuraishi ambao ndio kabila tukufu wangeweza kuzunguka Kaaba wakiwa wamejifunika shuka / nguo fulani, lakini makabila mengine yote yalitakiwa kuzunguka wakiwa uchi. Hivyo kwa ujio wa Mtukufu Mtume s.a.w. ibada hii ikarejeshwa kwenye uasili wake, ujahili na ushirikina ukaondolewa bali ikafanywa kuwa nzuri zaidi kwa kuongezwa baadhi ya mambo muhimu sawa na zama zake.

Hija ni ibada ambayo mtu analazimika kuifanya mara moja maishani mwake iwapo atakuwa na uwezo wa kufanya hivyo:

.... Na kwa ajili ya Allah watu wafanye Haji kwenye Nyumba hiyo - awezaye kufunga safari kwenda huko; 3:98

Kwa 'awezaye' inayo maana pana sana: ambayo ni kuweza kukamilisha mambo yote yatakayomuwezesha hujaji aweze kufika Makka na kurudi salama. Mali, nguvu, afya, na amani ya njia. Iwapo mtu hana uhakika na usalama wake halazimiki au tuseme hatakiwi/ haruhusiwi kuhiji.

Basi kwa kifupi hija hufanywa kwenye siku maalum kuanzia mwezi 8th of *Dhul-Hijjah*, ambao ni mwezi wa 12th wa kalenda ya kimwezi ya Kiislam, hadi 12th or 13th ya mwezi huo huo. Kuna matendo mengi ambayo hufanyika wakati wa Hijja, lakini ni muhimu yote yachukuliwe yenye kuashiria hekima na falsafa fulani ya ndani ya kiroho (ambapo kimsingi ni kumsaidia mwenye kuhiji kumkumbuka na kumuomba sana Allah) badala ya kuchukuliwa kuwa ni mambo ya dhahiri tu.

Mambo hayo ni:

Ihram ambayo ni kuvaa shuka nyeupe zisizoshonwa na bila kufunika kichwa kwa wanaume na kutokujifunika uso kwa wanawake. Wanawake wanaweza pia kuvaa nguo zao za kawaida maadamu tu hawatojifunika nyuso. Katika Ihram mahujaji hawaruhusiwi, kupunguza nywele, kukata kucha, kujipaka manukato, kuwinda, kukutana mtu na mke wake.

Ikimaanisha kwamba ni ishara ya kuyauwa matamaniuo yote ya dunia, usawa wa wanadamu, kukumbushia maisha yajayo na kuanza na moyo safi katika safari ya kumwendea Mungu.

Wakiwa kwenye hali hiyo ya Ihram mahujaji hutakiwa hukimbilia kuingia kwenye eneo takatifu (Haram) ambalo ni mzunguko wa kati ya kilomita 7.5 hadi 22 kuzunguka Kaabah. Kwenye eneo hili hujaji haruhusiwi kuleta uvunjifu wowote wa amani kiasi hiki kwamba hata kukata kitawi cha mti hakuruhusiwi, ili kila kitu kibaki kwenye amani.

Mara baada ya kuvaa Ihram Hujaji hutakiwa kuanza kusoma maneno yafuatayo ambao huitwa Talbiyyah:

Labeikka Allahumaa Labaika, Labaika la shariika laka Labaika, Innalhamda Waniimata Laka Walmulka, Laashariika Laka

Talbiyyah huanza kusoma tangu hatua ya kwanza hujai aanzapo ibada ya hija baada ya kuvaa Ihram hadi mwezi 10th *Dhul-Hijjah* ambapo mahujaji huchinja mnyama wa dhabihu.

Pia baada ya kuvaa Ihram mahujaji husali rakaa mbili na kuelekea Makka. Waingiapo hapo na baada ya kupata makazi yao, huelekea panapo kaaba kwa lengo la kufanya Tawafu ya kuwasili, *Tawaf-e-Qudum*.

Haujaji huanza Tawaf yake mahala penye jiwe jeusi lisilo chongwa (lisilo na sura maalum) ikiwezekana huanza tawafu yake kwa kulielekea na kulibusu jiwe hilo jeusi na hutufu mara saba, huku wakisoma Talbiyya kwa moyo wote.

Hakuna ibada ifanywayo kwa ajili ya jiwe hilo jeusi kama wadhanivyo baadhi ya wapinzani wa Islam. Jiwe jeusi inasemwa ndilo jiwe lililobaki kutoka kwenye ujenzi wa Nabii Ibrahim na mwanawe Ismil, ambao walijenga kwa mawe, likiashiria umoja wa Allah kwa kutokuchongwa kwake.

Hivyo kulibusu jiwe hilo na kuzunguka kaaba kuna ishara ya Mapenzi ya Umoja wa Allah ambao maisha yote ya Mwislamu hutakiwa yazunguke mapenzi ya Mungu.

Mara saba pia huonesha ukamilifu. Siku saba za wiki, mbingu saba, sura faatiha aya 7, jahannam milango saba n.k. hivyo kutufu mara saba inaonesha ukamilifu wa Mapenzi ya Mungu kila siku maisha yote ndipo mtu apate kusamehewa dhambi zake zote.

Pia ina maana ya kuzilinda hisi zake zote saba: kuona, kusikia, kunusa, kuonja, kugusa, lakini pia maumivu na joto au baridi (temp).

Matukio mengine ni Kusai (kukimbia baina ya safa na Marwa), ikiiashiria tukio la Bibi Hajira kukimbia baina ya vilima hivyo wakati alipokuwa akihangaika kumtafutia maji mtoto wake mchanga. Na Allah akaleta mabubujiko ya chemchem ya Zamzam. Ikimaanisha kwamba safari ya kumwendea Mungu inahitaji mahangaiko makubwa ya kutafakari na kuwaza, na kuomba, na kujitahidi kwa kila njia ya dhahiri (ibada) kwa kadri ya juhudi yako na kamwe usikate tamaa .

Siku ya 8th *Dhul Hijjah*. wakiwa kwenye Ihram mahujaji huelekea Mina. Hapo hupiga kambi hadi asubuhi ya pili, wanasali sala zote tano kuanzia Adhuhuri hadi alfajiri ya siku ya pili. Hapo Minaa mahujjai hutakiwa kutumia muda wao wote kwa ajili ya kumkubmuka Allah na kumuomba.

Siku inayofata 9th *Dhul Hijjah*, ambayo ndiyo huitwa hasa siku ya Hija, mara baada ya sala ya Alfajiri wanatoka Mina kuelekea viwanja vya Arafat. Hapo kipo kilima maarufu *Jabal-e-Rahmat*, ambapo Mtukufu Mtume s.a.w. alitoa hotuba yake ya mwisho.

Itaendelea Toleo Lijalo. Inshallah

Historia fupi ya marehemu mzee Lemu Abdallah Mnyite

Na Mwl. Hassan Mrope pamoja binti wa Marehemu.

Mzee Lemu Abdallah Mnyite alizaliwa huko Chitandi kijijini mnamo mwaka 1939. Kijiji cha Chitandi kipo wilaya ya Newala katika Mkoa wa Mtwara. Wakati wa udogo wake hakubahatika kwenda shule ya msingi, hata hivyo kupitia juhudi yake kubwa aliyoifanya katika kujifunza kusoma - kisomo chenye manufaa (Ngumbaru) Mzee Lemu alijiendeleza sana na akawa msomaji mzuri wa vitabu vya aina mbalimbali pamoja na magazeti ya kiswahili. Hali hiyo ya kujua kusoma na kuandika imeendelea hadi mwisho wa maisha yake.

Katika wakati wa ujana wake alipata kufanya kazi katika kampuni ya kujenga reli (Tanzania Rail Way). Kwa muda wa miaka sita (6) alifanya kazi hiyo hadi pale shughuli za kampuni hiyo zilipokwisha. Katika maisha yake ya ndoa alibahatika kufunga ndoa tano (5) kwa nyakati tofauti. Kwa ndoa zake hizo tano alibahatika kupata jumla ya watoto kumi na saba (17) kati ya hao watoto 17, kuna watoto 9 ambao bado wapo hai na wengine wanane (8) ambao tayari wamesha tangulia mbele ya haki mapema kabla ya baba yao kufariki.

KUJIUNGA KATIKA JAMAAT AHMADIYYA.

Mzee Lemu Abdallah alijiunga katika Jamaat Ahmadiyya mnamo mwaka 1966 aliyoipokea kutoka kwa Mzee Saidi Khatibu wa hapo hapo Chitandi. Alibaki kuwa Mwanajumuiyya Imara licha ya kupata misukosuko mingi.

Kitendo cha Mzee Lemu kujiunga katika Ahmadiyya, kilizua uhasama na uadui mkubwa kutoka kwa ndugu zake wa damu na ukoo wake kwa jumla ambao wapo Mahuta, Mnyambe, Mitene na wengine wa huko Manyombya takriban ndugu zake wote walimtenga. Baada ya kutengwa na nduguze wa damu, Mzee Lemu alibaki na ndugu wa kiroho ambao ni Waahmadiyya tu. Kila aina ya ushauri aliupata toka kwa Waahmadiyya. Hata alipougua au kuuguliwa na watu wa familia yake ni Waahmadiyya tu ndio walikuwa wasaidizi wake.



Mzee Lemu Abdallah Mnyite

Lakini jambo la kushangaza ni kwamba hao nduguze wa damu ambao wameshamtenga, kila walipopatwa na matatizo au misiba basi mzee aliendeela kuwasaidia kwa hali na mali bila kujali uadui na bughudha walizonazo dhidi yake.

Mzee Lemu alipenda sana ibada na aliwahimiza watu wafamilia yake wadumishe ibada za aina zote. Alikuwa mpole sana asiye na maringo na mara kwa mara aliwahimiza watoto na wajukuu zake kuwa wanyenyekevu wenye tabia njema. Pia alikuwa msafi wa mwili na mavazi, pamoja na nywele hadi meno meupe yaliyoonekana mara nyingi kwa vile alivyokuwa mcheshi.

Pia alipenda sana kuhubiri kiasi kwamba alihubiri watu wa rika zote, majirani alipokuwa na afya aliwahubiri. Alipenda sa kusoma vitabu vya Jamaat na kuwahimiza ahali zake wasome kwa bidii ili waweze kujibu hoja pindi wanapokutana na wasio wanajumuiyya. Kila alipomaliza sala ilikuwa ni desturi yake kuchukua kitabu chochote cha dini au gazeti la Mapenzi ya Mungu na kusoma.

Alikuwa mcheshi na alipenda majirani zake. Hakuwahi kugombana na mtu yeyote katika maisha yake hivyo alipendwa na watu wa rika zote. Alidumu kutenda mambo mema mpaka siku ya mwisho yake. Akiwa karibu kukata roho alitamka haya; "Ewe Mola wangu usiniache peke yangu, ewe Mola wangu nisamehe, ewe Mola wangu niondolee maumivu". Na aliyarudia rudia maneno hayo mpaka umauti unamfika.

Mzee Lemu ameugua kwa muda mrefu na kulazwa mara kadhaa katika hospitali ya Wilaya ya Newala. Kwa mara ya mwisho alilazwa hospitalini hapo tarehe 10/09/2016, lakini baada ya siku mbili tu, akafariki siku ya Jumatatu tarehe 12/09/2016.

Jambo jingine la kushangaza ni kwamba wale ndugu wa damu ambao kwa miaka mingi walishamtenga walihudhuria kwa wingi sana katika mazishi yake yaliyofanyika tarehe 13/09/2016. 'Inna lillahi wa inna ilaihi rajiuun'.

Marehemu ameacha mjane mmoja na watoto tisa. Mwenyezi Mungu Amlaze mahala pema peponi. Amin.

بسم الله الرحمن الرحيم

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA TANZANIA

KALENDA YA MATUKIO KWA MWAKA (JULAI 2016 - JUNI 2017

MWEZI	MWAKA	TAREHE	TUKIO
JULAI	2016	01 – 10	Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa – Dar es Salaam.
		11 – 16	Siku maalum za kukutana na viongozi wa serikali/waandishi wa habari sehemu walipo kwa lengo la kuleta uhusiano nzuri.
		7	**Sikukuu ya Eid Ul Fitri***
		18 – 25	Siku maalum za makusanyo ya michango ya Waqf-e-Jadid na Tahrik Jadid
AGOSTI	2016	1 – 8	Maonyesho ya Kilimo kitaifa - Mikoa husika
		12 – 14	**Jalsa Salana Uingereza**
SEPTEMBA	2016	1 – 10	Siku maalum za maonyesho ya vitabu katika Mikoa husika.
		07 – 14	Wiki maalum ya kuchanga mchango wa mkutano wa mwaka (Jalsa Salana)
		20 – 21	Uendeshaji wa semina za Tabligh katika kila tawi.
		13	**Eid Ul Adhha***
		30	**Jalsa Salana Tanzania**
OKTOBA	2016	1-2	
		24	Siku ya mwisho ya kupokea ripoti za makusanyo ya Tahrik Jadid 2015/16
NOVEMBA	2016	7-8	**Siku maalum za mahubiri nchi nzima.** Mahubiri yafanyike, viongozi wote wa Matawi ni lazima washiriki, ripoti itumwe Makao Makuu.
		16 – 30	Ahadi za Tahrik-e-Jadid kwa mwaka mpya (Novemba 2016 / Oktoba 2017)
		27	**Siku ya waanzilishi wa dini.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii hii).
DISEMBA	2016	01 – 15	Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya Waqf-e-Jadid.
		17 – 18	Ijtimaa ya Ansarullah Kitaifa - Dar es Salaam
		24 – 25	Siku maalum za Tarbiyyat Kitaifa. (Msukumo uwekwe zaidi kwa Waahmadiyya wapya).
JANUARI	2017	13 – 20	Ahadi mpya za Waqf-e-Jadid kwa mwaka 2017.
		22	Mitihani kutoka Kitabu cha: **Toeni Fatwa**
		23 – 30	Siku maalum za makusanyo ya mchango wa kawaida.
FEBRUARI	2017	01 – 06	Siku maalum za kuwaalika wageni kwa mazungumzo katika Jamaat zote. Taarifa zitumwe Makao Makuu.
		20	**Siku ya Mwana Aliyeahidiwa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
		25 – 26	Siku maalum za kuwatembelea wagonjwa, mahospitalini na majumbani. Pia kuwatembelea mayatima, walemavu, na vikongwe (washiriki, Ansar, Khuddam na Lajna).
MACHI	2017	03 – 12	Siku maalum za kufanya vikao vya kujadiliana ajenda za Shura ya 2017 na kuchagua wajumbe.
		13 – 14	Mahubiri Maalum kwa kila tawi. (Viongozi wote ni lazima washiriki).
		19	Mahubiri ya tarehe 13 – 14 yatolewe maelezo yake mbele ya Wanajumuiya wote.
		23	**Siku ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
		31	Siku ya mwisho ya kutuma dondoo za Mushawara kutoka matawini kwa ajili ya Shura ya mwaka 2017.
APRILI	2017	09	Mitihani kutoka kitabu cha: **Kigezo cha Dini**
		09 – 16	Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya mchango wa Tahrik Jadid na Waqfe Jadid.
		29-30	**Shura ya Kitaifa Dar es Salaam – mwaka 2017.**
MEI	2017	09 –16	Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya michango. (Hasa mchango wa kawaida).
		12	Wajumbe wa Shura wayaeleze matawi yao maazimio ya Shura - 2017
		25	**Kuanza kwa Saumu ya Ramadhani**
		27	**Siku ya Ukhalifa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii hii).
JUNI	2017	01 – 15	Siku maalum za kuhakikisha kwamba kila Mwanajumuiya amekamilisha Bajeti ya michango yake hasa wa kawaida/Wasia sawa na kiwango cha kila mwezi. Juhudi maalum zifanywe.
		23	Mitihani kutoka kitabu cha: **Hotuba ya Lahore**

***Zingatia: Saumu ya Ramadhani, na Sikukuu zote mbili zinategemea kuandama kwa mwezi.**

Kiini cha Waqfu Nau

Kutoka uk. 11

hapo wao ni maalum. Kama wanakuwa msitari wa mbele kuutii Ukhalifa na kutekeleza maamuzi yake, hapo wanakuwa maalum. Wanakuwa hasahasa maalum kama wao ndio ambao wanakuwa imara na wenye kujitolea kushinda wengine. Wanakuwa maalum sana kama watakuwa mbele sana katika upole na kutokuwa na ubinafsi, chuki na majivuno na wanapigana Jihad dhidi ya hilo. Wanakuwa maalum kama ni miongoni mwa wale wanaosikiliza hotuba zangu na wanaangalia vipindi vyangu vingine kwenye MTA ili wadumu katika kupata muongozo. Kama wakitekeleza haya na mambo yote yale yanayopendwa na Allah na wakijiepusha na vitu vyote vile ambavyo Allah Amevikataza, basi hapo wao ni maalum sana na kipekee. Vinginevyo kunakuwa hakuna tofauti kati yao na wengine.

Hili ni lazima likumbukwe na wazazi pia kwamba wawafundishe watoto wao katika mistari hii: kama mambo haya yapo, basi, Allah Amewafanya nyie kuwa chanzo cha kuleta mapinduzi duniani. Kama sio hivyo na dunia haiwaangalii ninyi kama mfano bora, basi, kuna nini katika kuzungumzia kuwa maalum, hapo Machoni pa Allah, watahesabika miongoni mwa wasio na imani na wavunjao ahadi. Hivyo, katika kuwapitisha katika harakati za mafunzo, wazazi wana wajibu wa kuwafanya hao maalum, na, wakikua, Waqfiin Nau wao wenyewe wafikie cheo hiki cha kuwa maalum. Kama nilivyosema kwamba wakati wa kupitia hatua mbali mbali za elimu ya dini na kidunia, iulize Jumuiya ni njia ipi uifuate au muamue nyie wenyewe. Nimesema hapo kabla kwamba wavulana wa Waqfu Nau watoe kipaumbele cha kwanza kwenda katika Jamia ili kuwa Shekhe au Mhubiri. Ndio hitajio la sasa. Jumuiya inapanuka. Jumuia mpya zinafanyika sio tu katika nchi ambako Jumuiya ilianzishwa siku nyingi kabla, lakini Allah Anaipa Jumuiya nchi mpya pia, na Jamaat zinaanzishwa kule. Na, katika kila nchi, tunahitaji idadi kubwa ya mashekhe na wahubiri.

Kisha, tunahitaji madaktari kwa ajili ya hospitali zetu. Pakistani, tunahitaji madaktari wengi waliobobea katika maeneo tofauti tofauti. Madaktari wanahitajika Qadiani kwa ajili ya Hospitali. Kama hawawezi kwenda kutokea hapa, kwa kuwa watu wanasikiliza hotuba zangu duniani kote katika nchi zao, Waqifiin Nnau waweke zingatio kwenye hili. Tunahitaji madaktari bingwa. Kuna pengo kubwa, tuna mabingwa wachache. Madaktari wanahitajika Afrika katika nyanja zote. Kwa kuwa tunajenga hospitali kubwa huko Guatemala, madakatari wanahitajika huko na wanaweza kwenda huko kutokea Kanada. Katika siku za usoni, tunawahitaji huko Indonesia. Mahitaji yatakua kadiri Jamaat inavyopanuka. Watoto wa Waqifiin Nau ambao wanakuwa madaktari, waje, wabobee, wapate elimu ya juu na uzoefu kutoka katika nchi hizi, na waende katika nchi ambazo ni rahisi zaidi kwenda. Jileteni na Jamaat itawapeleka. Hali kadhalika, walimu wanahitajika kwa ajili ya shule. Wote wavulana na wasichana wanaweza kufanya kazi kama madaktari na walimu. Kwa hiyo, wekeni mazingatio kwenye hili. Pia tunahitaji wasanifu majengo na wahandisi ambao ni mabingwa wa ujenzi, ili waweze kuokoa fedha za Jamaat kwa kufanya michoro mizuri zaidi na kusimamia kazi za ujenzi kwa ajili ya misikiti, nyumba za Jumuiya, shule, hospitali n.k. Vifaa vizuri zaidi vinaweza kupatikana kwa kutumia fedha kidogo. Kisha, tunahitaji wafanyakazi wa kuwasaidia madaktari pia. Nao pia wajiunge. Hizi ni idara chache za muhimu ambazo Jamaat inazihitaji sasa. Mahitaji ya baadae pia yatabadilika sawa na hali.

Waqfiin Nau huwa wanapendelea zaidi maeneo fulani, na wanaponiuliza, huwa nawaruhusu kusomea, nikijali mapendeleo yao. Lakini, hapa, ningewashauri wanafunzi kwamba wajifunze utafiti wa fani mbalimbali za sayansi pia. Na katika hili, kwa ujumla, wote Waqifiin Nau na wanafunzi wengine wanahusika. Kama, katika idara mbalimbali za sayansi, wanasayansi wetu bora kabisa watapatikana, basi, katika siku za usoni, ambapo Waahmadiyya watakuwa wanafundisha elimu ya dini na dunia itatutegemea sisi kujifunza kuhusu dini; kutakuwa na Waahmadiyya ambao watakuwa wanafundisha elimu ya dunia pia. Katika hali hiyo, bila shaka, Waqfiin Nau watakuwa wakifanya kazi duniani, lakini lengo lao litakuwa kuthibitisha umoja wa Mungu duniani kupitia elimu na kazi zao na kueneza dini Yake.

Hali kadhalika, Waqfiin Nau wanaweza kuingia katika idara zingine, lakini lengo lao la msingi ni lazima ijulikane kwa wote kwamba ninyi ni Waqfu Zindagi na, kama, wakati wowote, mnatakiwa kuacha kazi za kisekula na mjitoe ili kufanya kazi ya dini, basi mtakuja bila kutoa visingizio vyovyote. Jambo la muhimu ambalo kila waqfu Nau ni lazima alikumbuke ni kwamba ruhusa ya kufanya kazi za kisekula imetolewa kwao, lakini isiwe ni aina ile ya kazi ambayo itawanyima kufanya ibada ya Allah na elimu na kuhudumia dini; bali kupata viwango vyao vya juu iwe ndio kipaumbele chao cha kwanza. Kujifunza maelezo ya Qurani Tukufu na vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa (AS), ni lazima kwa kila Waqfu Nau. Silabasi ambayo pengine imetengenezwa mpaka kwa umri wa miaka 21, na idara ya waqfu Nau ipo. Baada ya hiyo, ni lazima kuongeza elimu yenu ya dini.

Ninataka kuwaambia wazazi kwamba haijalishi kiasi gani cha mafunzo wanatoa kimdomo, itakuwa haina mashiko kama maneno yao na vitendo vyao haviendani na hilo. Wazazi ni lazima watengeneze vizuri hali zao za kusali. Ni lazima waanzishe taratibu za kusoma na kufundisha Qurani Tukufu. Ni lazima wawe mfano bora wa imani ya juu. Wao wenyewe inawajibu wageuke kupata elimu ya dini. Viwango vya juu vya kuchukia uwongo lazima vipatikane. Pamoja na dhara lililofanywa kwa baadhi na viongozi, ni lazima wajizuie kuzungumza majumbani mwao, dhidi ya mfumo wa Jamaat au viongozi. Kwenye MTA, angalau hotuba zangu ni lazima ziwe zinasikilizwa kila mara. Mambo haya ni ya lazima sio kwa wazazi wa Waqfiin Nau peke yao. Bali, kila Muahmadiyya, ambaye anataka vizazi vyake vya baadae viungane na Jamaat, aifanye nyumba yake kama ni nyumba ya Muahmadiyya na sio nyumba ya wasaka dunia. Vinginevyo vizazi vijavyo, vikiwa vimemezwa kwenye dunia, sio tu kwamba vitakengeuka kutoka kwenye Ahmadiyya, lakini watakengeukia mbali na Mungu na wataangamizwa dunia hii na Akhera. Mungu Akipenda, sio tu watoto wa Waqfu Nau ndio wawe wa kupata ukaribu na Allah na kutembea kwenye njia ya Taqwah bali na vitendo vya wapendwa wao ni lazima pia viwe ni vya kuwaokoa dhidi ya kuwapatia majina mabaya. Kila Muahmadiyya ni lazima awe ni Yule Muahmadiyya safi ambaye amepata mwanga wa kiroho wa Masihi Aliyeahidwa (AS), tena na tena. Hivyo, kwamba, hivi karibuni, tuone bendera ya Ahmadiyya na Islam ya kweli ikipepea duniani.

Masihi Aliyeahidiwa (AS), anasema katika nukta hii, "Mtu, kwa kufanya tendo moja au mawili, anafikiri kwamba amemridhisha Allah. Kwa hakika, hali siyo hiyo. Utii ni kazi ngumu sana. Utii wa masahaba (ra) ulikuwa ndio utii. Ule ulikuwa utii hasa. Hivi utii ni jambo rahisi? Mtu ambaye hatii kabisa kabisa, analeta jina baya kwa mfumo huu. Hakuna amri moja tu. Kuna amri nyingi. Kama ilivyo milango mingi ya peponi, kwamba mtu mmoja anaingilia mlango fulani na mwingine anaingilia mlango mwingine. Hali kadhalika, Jahanamu ina milango mingi. Hali isije ikawa ile kwamba unafunga mlango mmoja wa Jahanam na kufungua mwingine". Anasema zaidi, "Baada ya kufanya Baiat, mtu hataishia kuamini tu kwamba mfumo huu ni wa kweli na kwa kuamini hivyo pekee, atabarikiwa. Allah Anaridhia tu kuamini! Sivyo, mpaka vitendo viwe vizuri. Kwa kuwa mmejiunga na mfumo huu, jaribuni kuwa wazuri, waadilifu, jiepusheni na kila ubaya, dumisheni ulimi laini, fanyeni kuomba msamaha kuwa ndio ada yenu, na nyenyekeeni katika maombi yenu". Allah, Mwenye Enzi, Atujaalie uwezo wa kutekeleza ushauri huu. Iwe kwamba sisi na vizazi vyetu lazima tuwe kwamba tunaganda kwenye matendo mema na Taqwah na ambao tunakamilisha kazi ya Masihi Aliyeahidiwa (AS). Amiin!

Ziara ya Amir sahib mkoani Shinyanga

Kutoka uk. 12

mafanikio na maendeleo makubwa katika maisha yenu.

Mwisho Amir sahib aliwahakikishia kuwa atajitahidi kuwaletea Mwalimu wa kudumu ili aje kukaa nao na awafundishe kwa urahisi na ukaribu juu ya mafundisho sahihi ya dini Tukufu ya Islam.

Baada ya khutba ya Amir sahib ilitolewa adhana kwa ajili ya sala ya Adhuhuri na baadae sala ya Adhuhuri iliongozwa na Amir sahib na baada ya sala chakula kililetwa kwa ajili ya waliohudhuria na baada ya chakula msafara wa Amir sahib ulielekea katika ziara ya tawi jingine.

ZIARA YA TAWI LA KASOMELA NA UWEKAJI WA JIWE LA MSINGI LA UJENZI WA MSIKIT MPYA.

Siku hiyo hiyo ya Alhamis tar. 26/5/2016 Amir sahib alifanya ziara nyingie katika tawi jipya la Kasomela wilayani hapo Ushetu na alifika tawini hapo Kasomela saa tisa na robo Alasiri na alilakiwa na wanajamaat waliojipanga katika msitari kwa ajili ya kusalimiana na Amir sahib, na baada ya kusalimiana sherehe za hafla hiyo zilianza kwa usomaji wa Qur`an Tukufu iliyosomwa na mwl Abdullah Difika kasha ilifuatiwa na risala ya tawi kwa Amir sahib iliyosomwa na Katibu wa tawi hilo.

Katika risala hiyo walisema kwamba; Sisi waumini wa Kasomela tulianzisha kuuinua Uislam katika kijiji hiki mwaka 2007 na tulijenga Kibanda swala, baadae tukalima shamba la Waislam na baadae tukaweka mfuko wa Waislam hatimaye tukajenga msikiti wa muda wa matope na tukaezeka mabati. Amir sahib kilio chetu kikubwa ni kukosa Mwalimu wa kutuongoza, awali tulikuwa tunasali sala za kawaida na tukawa tunaomba kwa Allah ili tupate mtu wa kutuongoza na pia Mungu atushushie neema ili yapatikane mabadiliko. Baadae risala hiyo waliikabidhi kwa Amir sahib.

Baadae alisimama Mwenyekiti wa kijiji aliyesema kuwa anajisikia furaha na faraja kwa kupokea wageni wa Mungu na hivyo anawakaribisha sana.

Pia alisimama Mtendaji wa Kijiji ambaye baada ya salamu alisema tunashukuru kupata wageni hawa, hivyo ndugu zangu wananchi nawaomba tuwasikilize kwa makini ili tupate faida na baraka walizokuja nazo.

Pia alisimama Mwl. Mkuu wa Shule ya msingi Kasomela ambaye baada ya salamu alisema kuwa kupata wageni ni neema kubwa hivyo tuna imani mabadiliko ya kweli yatapatikana.

Pia alipata fursa Mchungaji wa kanisa la Roman Catholic ambaye baada ya salamu na shukurani yeye alisema kuwa amefika hapa kwa kutambua umuhimu wa ushirikiano wa kidini, kwani ushirikiano utaleta maendeleo ya kweli na ndio maana sisi tumekuja kuungana na wenzetu Waislam.

Baadae alisimama Mwenyekiti wa CCM wa Kata ambaye baada ya salamu na shukurani alisema nawapongeza Waislamu wa eneo hili kwa kushiriki na tumefurahi kufikiwa na kiongozi ambaye atatupatia mabadiliko ya kiroho na maendeleo ya kweli.

Hatimaye alisimama Amir sahib ambaye baada ya salamu, Tashahud na sura Faatiha aliwashukuru watu wote kwa kuhudhuria na aliwakaribisha katika hafla hiyo.

Aliwaambia kwamba ndugu zanguni tumekuja hapa kwa ajili ya uhusiano mzuri tulio nao baina yetu, miezi michache iliyopita nilipata taarifa ya kuwa hapa walikuja Wabashiri wetu na wakawapatieni ujumbe wa Masih Aliyeahidiwa a.s. nanyi mkaupokea na kuukubali na hatimaye mkajiunga na Jumuiya hii.

Aidha Amir sahib aliwafahamisha kuhusu Jamaat ni nini kama alivyofanya katika maeneo alikoanzia ziara yake hii na akawa amewaasa kwamba kwa kuwa mmeshajiunga na Jumuiya hii mnatakiwa kufuata mafundisho ya dini ili mpate mabadiliko ya kweli, kama kati yenu kuna mtu aliyekuwa anakunywa pombe aache mara moja, na kama kati yenu kulikuwa na mtu anayefanya maovu au mambo ya hovyo basi anatakiwa ayaache mara moja. Kumbukeni kuwa baada ya kujiunga na Jamaat mnatakiwa mjibadilishe kweli kweli ili muwe watu wema. Fahamuni kuwa mkifanya maovu mnakuwa mnaiaibisha Jamaat.

Mwishowe Amir sahib aliwaambia kuwa baada ya mazungumzo haya tutaweka jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa Msikiti mpya na siku chache zijazo msikiti huo utakuwa umekamilika. Sasa msikiti huo ukishakamilika ni juu yenu kuujaza na kuustawisha na milango yake itakuwa wazi kwa wote hata Wakristo wanaruhusiwa kuja kusali maadamu wanafanya ibada ya Allah. Baada ya hapo sala ya Alasiri ilisaliwa na baadae Amiri sahib aliongoza uwekaji wa jiwe la msingi na baadae maombi yaliongozwa na Amir sahib kisha ilifuatiwa na chakula na baadae saa kumi na mbili kamili msafara wa Amir sahib uliondoka kijijini hapo kuelekea Kahama.

ZIARA YA MWISHO TAWI LA SUNGAMILE NA SALA YA IJUMAA.

Amir sahib aliingia hapa Sungamile na kupokelewa na wanajamaat wa Sungamile na baada ya kusalimiana na wanajamaat aliingia msikitini ambapo alifanya kikao cha pamoja na waalimu waliopo mkoani Shinyanga, kikao hicho kilidumu kwa masaa mawili na nusu. Kilipoisha kikao ilitolewa Adhana kwa ajili ya sala ya Ijumaa ambayo iliongozwa na Amir sahib ambapo pia katika khutuba ya Ijumaa aliwaasa wanajamaat kujiimarisha ndani ya Jamaat na kujitahidi kufuata nidhamu na taratibu za Jamaat ili wapige hatua ya maendeleo ya kiroho. Aliwaasa wanajamaat wa hapo kujiepusha na siasa kwenye dini na wawe tayari kupokea maamuzi ya Jamaat yanapokuwa yametolewa kwa ajili yetu na hatuna haki ya kuhoji juu ya maamuzi ya Jamaat bali tunatakiwa kuwa *'Samiina wa atwaana'* yaani tunasikia na tunatii.

Baada ya sala ya Ijumaa Amir sahib aligawa zawadi za vitabu kwa wageni waalikwa wa serikali waliokuja kumsalimia, zawadi hizo ziliandaliwa na wanajamaat wa Sungamile.

Baada ya hapo Amir sahib pamoja na msafara wake walikaribishwa kupata chakula nyumbani kwa raisi wa Tawi la Sungamile kilichoandaliwa na rais wa tawi bwana Shaaban Karanga.

Baada ya chakula Amir sahib pamoja na wajumbe wake walipata fursa ya kusikiliza Khutba ya Ijumaa ya Huzuur Aqdas (atba) kupitia MTA live. Na baada ya kumalizika khutuba Msafara wa Amiri pamoja na wajumbe wake uliondoka hapo Sungamile kuelekea Shinyanga mpaka Mwanza na hapo ndipo ziara ya Amir sahib kwa mkoa wa Shinyanga iliyodumu kwa wiki moja ikawa imekwisha.

Mwisho.

Kiini cha Waqfu Nau

Kutoka uk. 12

Hawapo kwa ajili ya dunia. Ahadi aliyoishika mama yake kabla ya kuzaliwa kwake, maombi aliyoyaomba kabla ya kuzaliwa kwake na malezi aliyofunzwa, amelelewa kwa namna ambayo atachagua dini badala ya mambo ya kidunia. Amepata bahati nzuri kwamba Allah amesikia maombi ya mama yake na amesaidia juhudi za malezi yake zitoe matunda. Sasa, bila ya matamanio na shauku yoyote ya dunia, anaahidi yeye mwenyewe kuihudumia dini na Imani tu.

Kuwafahamisha juu ya dhamira ya Waqfu nau ni muhimu sana katika umri wa miaka 15, wakati wanapoandika tena ahadi zao za Waqfeen. Katika jambo hili nimetoa maelekezo kwa uongozi kwamba ni lazima tupate kauli zao kwa maandishi wanapofikisha umri wa miaka kumi na tano (15) kama wanahitaji kuendelea na waqfu wao. Katika umri wa miaka 15 au 21 wale wote ambao hawajajiunga na Jamia ni lazima waandike tena ahadi zao kwa maandishi mara baada ya kumaliza elimu zao. Na katika kipindi cha katikati pia ikiwa anataka kujiunga na fani nyingine ni lazima aandike tena ahadi yake. Ili katika kila hatua sawa na utashi wa moyo wake aeleze kama anahitaji kuendelea na Waqfu wake.

Kulihusu hili, kama nilivyosema, hakuna mtoto yeyote wa Waqfu Nau anayetakiwa kufikiria kuwa baada ya kushika ahadi ya kuwa Waqf, je ni namna gani watakavyoishi au wapate hofu kuwa ni jinsi gani wataweza kuwahudumia wazazi wao kifedha au kwa njia nyingine za kimwili. Siku chache zilizopita nilikuwa na darasa la Waqfu Nau. Mtoto mmoja wa kiume aliniuliza swali kuwa ikiwa watajitoa na kutumia muda wao wote katika kuitumikia Jamaat, Je watawezaje kuwasaidia wazazi wao kifedha, kimwili au kwa ujumla.

Uwepo wa swali hili unaonyesha ukweli halisi kwamba wazazi hawaingizi katika mioyo ya watoto wa Waqfu Nau kuwa wamewatoa kwa ajili ya jamaat na pia wao ni amana kwa ajili ya Jamaat tu. Ndugu zao watatoa huduma kwa wazazi badala yao. Katika maombi ya mama yake Mariamu neno “bila shaka” limetumika likionyesha kuwa alimtenga mtoto na majukumu ya kidunia na akaomba kuwa majukumu ya kidini ndio yawe kipaumbele kwake.

Kwa hiyo ninataka kuwaeleza wale kina Baba na kina Mama kuwa kusema tu Waqfu Nau haitoshi peke yake. Zaidi, mtu ajue Waqfu Nau ni jukum la muhimu sana. Ni jukum la wazazi hadi pale Waqfu Nau anapofikia utu uzima, pale ndio unapoweza kusema kwamba ni jukumu lake.

Zingatieni juu ya kauli ya Mtukufu Mtume(s.a.w) kuwa watazameni wenye hali ngumu kifedha zaidi yenu na watazameni walio juu kiroho zaidi yenu ili muweze kupiga hatua kwenye Mambo ya kiroho kuliko mambo ya kidunia. Hivyo wavulana Waqf Nau ambao wamemaliza masomo yao, wanatakiwa kuongeza viwango vya hali zao za kiroho zaidi ya hali ya kimwili na mambo ya kidunia. Masih Aliyeahidiwa (a.s) alitarajia kutoka kwa kila Ahmadiyya awe na viwango vya juu ya mambo ya kiroho. Mtu ambae wazazi wake wamemtoa kwa ajlili ya dini kabla ya kuzaliwa na wakamuombea yeye pia, Je ni kwa kiwango gani anatakiwa kujaribu ili kufikia viwango hivyo.

Masih Aliyeahidiwa(a.s) alisema, “Ninalifanya jambo hili kuwa ni jukumu langu na ninaweka Wasia kwa ajili ya Jamaat na kutuma ujumbe huu… ili hapo baadae kila mmoja ana haki kukubali au kukataa. Ikiwa mtu anahitaji uokovu na Anahitaji kuwa Mcha Mungu na kupata maisha ya milele, basi anatakiwa ayatoe maisha yake kwa ajili ya Allah. Na kila mmoja aingie katika njia hii ili kupata ile daraja na kiwango ambacho atasema maisha yangu, kifo changu, kujitolea kwangu na Ibada zangu zote hizi ni kwa ajili ya Allah mtukufu. Roho yake, iwe kama ya Ibrahim (a.s) na aseme:

“Nanyenyekea kwa Mola wa walimwengu”. (Sura 2:132)

Anasema, “Kama mtu atajipoteza kwa Allah na hajapata kifo kwa ajili ya Allah, hawezi kupata maisha mapya. Hivyo, enyi mliokuwa na uhusiano na mimi, hebu oneni kuwa mimi ninaliona jambo hili la kujitolea maisha kwa ajili ya Allah kuwa ni kiini na lengo la maisha yangu. Huu ndio msingi na huu ndio muendelezo. Jitafakarini wenyewe kuwa ni wangapi kati yenu wanaopenda kufanya jambo langu hili kwa ajili yenu wenyewe na kufanya kujitolea kwenu kupendwe na Allah”.

Hivyo, ili Waqfu Nau awe juu kuliko Waahmadiyya wengine anatakiwa kufikia viwango hivi. Wengine wanafanya Waqfu Nau kwa ajili ya Imani na kila mtu hawezi kuwa Waqfu. Allah anasema liwepo kundi miongoni mwenu, ambao watajifunza elimu ya dini na wataenda kwa wale walioshikamana na dunia kuwafundisha. Lakini pia jambo hili lilielezwa na Masih Aliyeahidiwa(a.s) kuwa Imani na kumuogopa Allah ni lazima liwe jambo la kipaumbele wakati wa kufanya shughuli za kidunia. Waqfu Nau wanatakiwa waongeze viwango yao vya Ridhaa na kujitolea.

Hawatakiwi kujidhani kwa kuwa wao ni dhaifu kifedha, hivyo ndugu zao wanawaona wao kuwa duni au wazazi wao hawatawazingatia kuliko wengine. Kwanza kabisa wazazi hawatakiwi kuwa na mawazo haya kwamba wanaojitoa kwa ajili ya Allah ni watu Duni. Wanatakiwa kuwa na mtazamo kuwa viwango na hali za Waqfu Nau ni vikubwa zaidi

Lakini Waqfu Nau wanatakiwa wajiweke wenyewe kuwa ni watu wanyenyekevu katika dunia hii. Waqfu Nau wanatakiwa kukuza viwango vyao vya kujitolea, maombi na imani zao. Wanatakiwa watumie vipawa vyao vyote na uwezo wao wote ili kutimiza ahadi za wazazi wao na ahadi zao. Jitahidini kushikilia imani zenu kuwa juu zaidi. Kisha baraka za Allah mtukufu hazitawaacheni bila ya malipo yake.

Kuhusiana na kutimizwa kwa ahadi hiyo, siku moja, Masihi Aliyeahidiwa (AS) alisema kwamba Mungu Amemsifia Hadhrat Ibrahim (as) ndani ya Kuruani tukufu. Kama alivyosema:

“Na kwa Ibrahim aliyetimiza amri” (53:38)

Kwamba alitimiza ahadi aliyoiweka. Kwa hiyo, kutimiza ahadi siyo jambo la kawaida. Na ahadi ya kujitolea maisha, ambayo kwayo tumesikia maneno yaujazayo moyo kutoka kwa Masihi Aliyeahidiwa (AS), ni kubwa ilioje ahadi hii! Kama kila mvulana na msichana wa Waqfu Nau atatimiza ahadi hii kwa uaminifu, tunaweza kuleta mapinduzi katika dunia hii. Baadhi ya vijana waliooana hivi punde huwa wanakuja kwangu na kusema, mimi ni Waqfu Nau, mke wangu ni Waqfe Nau na mtoto wangu ni Waqfu Nau au mama anasema kwamba yeye ni Waqfu Nau. Baba atasema kwamba yeye ni Waqfu Nau na mtoto wake ni Waqfu Nau. Ni jambo la kusifiwa; lakini itakuwa ni lenye faida kwa Jamaat hasa kama tu watatimiza ahadi zao kwa uaminifu.

Katika sehemu nyingine, akimzungumzia Ibrahim (as). Masihi Aliyeahidiwa (AS) ameelezea zaidi mada ya uaminifu. Anasema kwamba njia ya kupata ukaribu na Allah ni kuonyesha uaminifu Kwake, na daima kuwa mkweli. Uaminifu wako Kwake uwe wa kweli. Sababu kwamba Ibrahim (as) alipata ukaribu zaidi kwa Allah ilikuwa ni hiyo hiyo. Hivyo, Anasema:

“Na kwa Ibrahim ambaye alitimiza amri” (53:38).

Ikimaanisha kwamba Ibrahim ni yule Ibrahim, ambaye alionyesha uaminifu. Kuonyesha unyenyekevu, ukweli na uaminifu kwa Allah kunahitaji ‘kifo’. Sifa hii haiumbiki mpaka kwanza mtu awe tayari kuachana na raha zote na ladha za hii dunia na awe tayari kupata aina zote za kudharauliwa, shida na ufakiri kwa ajili ya Mungu. Kuabudu sanamu sio muradi wake mtu anaabudu mti au jiwe. Kila kitu kinachozuia kuupata ukaribu na Allah na ni chenye kupendwa zaidi Yake ni sanamu. Na, ana masanamu mengi katika nafsi yake kiasi kwamba hana habari ya ibada zake za masanamu. Katika zama hizi, katika baadhi ya sehemu, michezo ya kuigiza imekuwa masanamu, sehemu fulani intaneti ni sanamu, sehemu nyingine kuchuma kumekuwa sanamu na wakati mwingine matamanio mengine yamekuwa masanamu. Mtu anakuwa hajui kwamba yumo katika ibada ya sanamu na anaifanya bila kuonekana. Hivyo, (Masihi Aliyeahidiwa as) alisema, “Isipokuwa tu kama awe mukhlis kwa ajili ya Mungu na yuko tayari kukumbana na taabu zote katika njia Yake, rangi ya uaminifu na ukweli ni vigumu kuijenga. Ibrahim (as) hakupata jina lake burebure. Suati, “Na, kwa Ibrahim ambaye alitimiza amri” haikuja mpaka alipokuwa tayari kumtoa mtoto wake dhabihu. Allah Anataka vitendo na Anaridhishwa na vitendo; na vitendo vinakuja na maumivu. Mtu lazima ajitoe kufanya vitendo vya haki na kufanya vitendo vinavyomridhisha Mungu. Mtu lazima apitie huzuni na mateso. Lakini, (Masihi Aliyeahidiwa [as]) anasema kwamba ingawa kuna ugumu katika matendo lakini mtu huwa hayuko daima katika huzuni. Anasema zaidi kwamba kama mtu yuko tayari kwa ajili ya huzuni, basi, Allah Huwa hamuweki katika huzuni hiyo.

Alipokuwa akitii Amri za Allah, wakati Ibrahim alipokuwa tayari kabisa kumtoa mtoto wake, Mungu Alimuokoa mtoto wake. Maisha ya mtoto yaliokolewa na baba pia aliepushwa na huzuni ambayo ingekuwa imesababishwa na kumtoa mtoto wake. Alitupwa kwenye moto, lakini moto haukumdhuru chochote. Kama mtu yuko tayari kupata shida katika njia ya Allah, basi Allah Anamuepushia shida. Hiki ndicho kiwango tulichoambiwa na Masihi Aliyeahidiwa (as) tufyonze pendo la Allah na tupokee Baraka Zake na alitutegemea sisi kukifikia. Hiki ndicho kiwango ambacho kila Waqfi Nau sio tu kwamba ajaribu kukifikia lakini pia akumbuke kwamba mpaka pale kipimo chetu cha kujitolea kitakapopanda juu zaidi, madai yetu ya kujitolea maisha yatakuwa dhaifu. Baadhi ya kina mama wanaropoka kwamba wamekuja Kanada. Mtoto wao ni Murabi au Waqfu Zindagi huko Pakistan, mlete au mpangie hapa. Ajiunge nasi hapa. Wakati Waqfu umeshatolewa, sasa madai haya ni kwa sababu gani, matakwa haya ni kwa nini. Matakwa yalishafanywa tayari.

Kama nilivyokwisha sema, uelekeo wa kujiunga na Waqfu Nau unaongezeka. Hili linafurahisha sana. Imarisheni muelekeo huu, muufanye uwe mukhlis kwa ajili ya Mungu na wala msije kuwa wale wanaovunja au wanaodhaifisha ahadi zao kutokana na mabadiliko ya hali. Masihi Aliyeahidiwa (AS) alisema kwamba kujitolea hakuwezi kuwa bila kuwa na huzuni na mateso. Kama hali imebadilika, ni lazima tuivumilie, na hasa kwa wale waliojitoa kuwa Waqfu: au wazazi wamewatoa watoto wao nao (watoto hao) wakakubali kuendelea na Waqfu wao. Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba mtu anapokuwa tayari kufanya aina zote za Waqfu kwa ajili ya Mungu, basi Allah Anambariki. Allah Hamuachi na Anambariki sana mno. Allah Awafanye Waqfiin Nau wote na wazazi wao ambao wanaelewa ukweli wa waqf nau kutimiza ahadi zao na wawe wanaodumu kupanda viwango vya uaminifu.

Kwa kifupi, ninataka pia kuvuta fikira kuhusiana na baadhi ya mambo ya kiutawala na mpango kazi wa Waqfe Nau. Baadhi ya watu wanauliza maswali na baadhi ya Waqifiin Nau wana fikira potofu katika akili zao kwamba kwa kujiunga na Waqfu Nau wamepata kitambulisho kipya. Bila shaka kitambulisho kimefanyika, lakini kwa kitambulisho hicho hawatapata upendeleo usio wa kawaida katika kuhudumiwa. Kinyume chake, wanapaswa kutumia kitambulisho hicho kunyanyua viwango vyao vya kujitolea. Baadhi ya watu wanapenyeza katika akili za watoto wao wa Waqfu Nau kwamba wao ni watoto maalumu sana. Matokeo yake ni kwamba hata wanapobalehe, hii ‘kuwa maalum” inaganda katika akili zao. Maswali haya na mambo ya aina hiyo yamenifikia mimi hapa pia. Wanatupilia nyuma mantiki ya Waqfu na wanalifanya swala la Waqfu Nau kuwa lengo la maisha yao kwamba wamekuwa maalum. Baadhi yao wamejenga mtazamo katika mioyo yao kwamba kwa kuwa wamo katika Waqfu Nnau basi hawahitaji kuhudhuria mipango ya Nasirat na Lajna kama wao ni wasichana, na hawahitaji kuhudhuria mipango ya Atfal na Khuddam kama wao ni wavulana - wana tandhiim yao ya pekee. Hili ni wazo la makosa, kama mtu analo. Kiongozi yeyote, hata Amir Jamaat, ni mwanachama wa Tanzeem.

Kwa hiyo, kila Waqfu Nau, mvulana au msichana ni lazima akumbuke kwamba ni mwanachama wa tanziim zao sawa na umri wao na ni wajibu kwao kuhudhuria mipango yao, na kama mtu hahudhurii, basi Sadr wa Tandhiim husika atoe taarifa kuhusu huyo. Kama Waqfu Nau huyo haboresheki, basi mtoto, mvulana au kijana wa aina hiyo ataondolewa katika mpango wa Waqfu Nau. Naam, kama kuna mipango fulani ya Jamaat, Waqfu Nau, au mipango ya Tanziim, basi, kwa maelewano ya pamoja, muda wa mipango hiyo inaweza kupangwa kwamba Tanziim na Waqfu Nau wanafanya mipango yao bila kuingiliana na kusiwe na mgongano.

Waqfu Nau, kama nilivyosema ni maalum sana. Lakini wanapaswa kulithibitisha hilo kwamba wako mbele ya wengine katika mahusiano yao na Allah; ni hapo tu ndipo watakapoitwa ‘maalum’. Wataitwa maalum kama wana khofu ya Mungu zaidi kushinda wengine. Wataitwa maalum kama viwango vyao vya ibada ni vya juu sana mno kushinda wengine. Wataitwa maalum kama watakuwa wanasli sala za nafali pamoja na zile za faradhi. Ni alama ya kuwa maalum kama kiwango chao cha tarbiyat ni cha juu sana. Kuna tofauti ya wazi katika lugha zao na uzungumzaji. Inaonekana bayana kwamba kuna mtu aliyefundishwa ipasavyo ambaye anapendelea dini juu ya dunia. Hapo ndipo watakuwa ‘maalum’.

Kama ni wasichana, basi, nguo zao na hijabu ni alama ya elimu ya kweli ya Islam. Wengine watakapoiona, wataona wivu na watasema kwamba pamoja na kuishi katika mazingira haya, nguo zao na hijabu ni mfano mzuri kupita kiasi. Hapo watakuwa maalum. Kama ni wavulana, basi macho yao yatakuwa yanatazama chini kutokana na haya na hawata tangatanga kuelekea matendo ya dhambi. Hapo watakuwa maalum. Watakuwa maalum kama watakuwa wanatumia muda wao kujipatia elimu ya dini badala ya kuangalia vitu visivyo na maana kwenye intaneti. Kama muonekano wa wavulana utakuwa tofauti na wengine. Hapo watakuwa tofauti. Wavulana na wasichana wa Waqfu Nau wanaweza wakaitwa maalum kama watakuwa wanasoma Quran Tukufu, wanatafuta amri zake, na wanapozipata wanazitekeleza. Kama kwa kudumu wanashiriki katika mipango ya Tanziim na Jamaat zaidi kuliko wengine, hapo, watakuwa maalum. Ni cheo maalum kama watawazidi kaka na dada zao katika kuwahudumia wazazi wao vizuri na kuwaombea.

Wakati wa kutafuta mchumba, kama wataangalia dini badala ya mambo ya kidunia, na kisha kuendeleza mahusiano yao, na wanaweza kusema kwamba kwa kufuata maalekezo ya dini wao ndio ambao wanaendeleza mahusiano yao. Hapo wataitwa maalum. Ni maalum kama ni wavumilivu zaidi ya wengine wakati wa magomvi na fujo, sio tu kwamba wanajiepusha nayo, bali pia wanakuwa wenye kuleta amani. Kama, katika nyanja ya tabligh, wanakuwa mstari wa mbele kutekeleza jukumu hili,

Endelea uk. 10

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Saf./Rab1. 1438 AH | NOV./DIS. 2016 | Nub./Fat. 1394 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Hakuna yeyote anisaliaye isipokuwa Allah atanirudishia roho yangu ili nimrudishie salamu yule mwenye kunisalia .
(*Abu Dawud*)).

Khalifa Mtukufu aeleza kiini cha Waqfu Nau

Hadhrat Khalifatul Masih V(atba) alitoa hotuba hii ya Ijumaa tarehe 28th Oktoba 2016 katika msikiti wa Baitul Salam, Toronto huko Canada. Baada ya Tashahud na Surat Fatiha, Huzur(atba) alisema;

Kwa fadhila za Allah, hali ya kuwatoa watoto kwa ajili ya kuitumikia Jamaat inaongezeka. Ninapokea barua kutoka kwa wazazi kila siku. Katika baadhi ya siku, idadi ya barua hufikia Ishirini(20) hadi Ishirini na Tano(25). Katika barua hizo wazazi wanaomba juu ya watoto zao ambao bado hawajazaliwa waingizwe kwenye mpango wa Waqfu Nau. Wakati Hadhrat Khalifatul Masih IV(rh) alipoanzisha jambo hili, kwa kipindi kile lilikuwa sio jambo la kudumu, lakini baadae alilifanya la kudumu. Na Jamaat hususan kina mama walisema 'tumetii'. Miaka 12 au 13 iliyopita sawa na msisitizo wa Jamaat katika jambo hili, idadi ya Waqfu Nau ilizidi zaidi ya elfu 28 (28,000). Na kwa Baraka za Allah idadi yake inakaribia Elfu 61. Kati ya hao wavulana wapo Elfu 36 na waliobakia ni wasichana. Hivyo, kwa kadiri muda unavyoenda, ile hali ya watu kuwatoa watoto wao kabla ya kuzaliwa inaongezeka.

Ijapokuwa jukumu la wazazi haliishii tu kwenye kuwatoa watoto wao Waqfu kabla ya kuzaliwa. Bali wanakuwa na majukumu zaidi ya hapo awali. Hakuna shaka, kwamba malezi ya kila mtoto wa Kiahmadiyya ni jukumu la wazazi, na wazazi hutaka yaliyo mema kwa mtoto wao. Wazazi waliomtoa mtoto kwa ajili ya dini, wanahitaji Elimu yake ya sekula, malezi na elimu ya dini pia viwe vizuri. Lakini jambo hili linatakiwa likumbukwe kwamba, kila mtoto hususan Waqf Nau ana amana ya Jamaat juu yake. Malezi yake na njia za kumfanya kuwa kiungo bora katika Jamaat na jamii ni jukumu la wazazi. Lakini pia malezi ya watoto wa Waqfu Nau, elimu yao ya mambo ya kisekula na elimu ya dini zinatakiwa kuchukuliwa kwa umakini mkubwa na wakabidhiwe katika Jamaat baada ya kuwaandaa linakuwa jukumu lingine kwa sababu nyingine.

Kuwa, kabla ya kuzaliwa wazazi wanaweka ahadi kuwa yeyote atakayezaliwa awe wa kiume au wa kike, watamtoa kwa ajili ya dini ya Allah, ili kutimiza kazi ya mtumishi wa kweli wa Mtukufu Mtume (s.a.w) ambayo ni kazi ya kutimiza muendelezo wa muongozo wa kweli, ambayo ni kazi ya kukamilisha kusambaza mafundisho ya Islam katika dunia, ambayo ni kazi ya kusisitiza uelewa wa dunia juu ya kutimiza haki za Allah na ambayo ni kazi ya kusambaza mafundisho ya Kiislam juu ya kutimiza haki ya kila mtu ulimwenguni.

Hili sio jukumu la kawaida, kwamba wazazi wa mtoto hususan mama, fikiria kabla ya kumzaa mtoto wake anashika ahadi na Allah. Na wanaandika barua kwa Khalifa wa zama kwamba wanamtoa mtoto wao kwa ajili ya mpango wa Waqfu Nau na kushika Ahadi na Allah kama mama yake Mariamu.

"(Kumbukeni) aliposema mwanamke wa Imrani: Mola wangu, hakika nimeweka nadhiri Kwako aliyomo tumboni mwangu kuwa wakfu; basi nikubalie. Bila shaka Wewe ndiwe Usikiaye, Ujuaye".(3:36)

Ewe Mola wangu, chochote kilichopo katika tumbo langu, ninakitoa kwako. Sijui kama hicho ni cha kiume au kike, lakini chochote kiwacho, ni mapenzi yangu na maombi yangu kuwa awe ni mtumishi wa imani. Nipokelee matakwa yangu. Wewe ndiwe usikiaje na ujuae kila kitu, kwa hiyo pokea maombi yangu yaliyojaa unyenyekevu pia. Unajua kuwa maombi haya ni sauti kutoka moyoni mwangu. Hii ndio shauku ya kina mama kwa watoto wao kabla ya muda na inatakiwa kuwa hivyo kwamba mama wa Kiahmadiyya anapoweka ahadi ya mwanae kuwa Waqfu Nau na baba pia ahusihwe katika hilo.

Hivyo, wakati mama wa mtoto aliyejiunga na mpango wa Waqf Nau, anapoomba hivi, majukumu hayo yanatakiwa kuweka katika fikra za kina mama na kina baba kwa lengo la kutimiza Ahadi na kupokelewa maombi. Mtoto anaingizwa kwenye mpango wa Waqfu Nau kwa makubaliano ya baba na Mama.

Allah Mtukufu Hakuhifadhi maombi haya katika Qurani tukufu kwa lengo tu la kusimulia habari za wakati uliopita. Lakini, Allah aliyapenda sana maombi haya hadi akayahifadhi kwa ajili ya kina mama wa baadae pia, ili kuwafanya watoto wao kuwa watu ambao watajitolea kwa kiwango cha juu kabisa katika imani kupitia maombi haya. Kila ombi la Imani lina lengo la kushika ahadi zaidi ya mambo ya kidunia, lakini Waqfeen anatakiwa kwenda juu zaidi ya viwango hivi. Hivyo nini ambacho wazazi wanachotakiwa kukiingiza katika ufahamu wa watoto wa Waqfu Nau tokea mwanzoni ni kwamba wao ni watoto wa Waqfu Nau na wazazi wao wamewatoa kwa dhati kabisa kwa ajili ya kuhudumia dini.

Na hili ndio lengo la maisha yao na wanatakiwa wafanye maombi pia, kisha watoto watakua wakiwa wanafahamu kuwa wanatakiwa wafanye kazi kwa ajili ya dini. Hawatakuwa wanakua wakifikiria kuwa wafanya Biashara au wanamichezo au kwenda katika fani nyingine. Bali watasema kuwa wao ni Waqfu Nau na hivyo ni Jamaat au Khalifa tu ndio wa kuwaambia fani gani wachague.

Endelea uk. 11

Ziara ya Amir sahib pamoja na ufunguzi wa Misikiti minne mkoani Shinyanga

Na MWL. SHAABAN S. LUSSEZA - Shinyanga

Kutoka toleo lililopita.

Baade alisimama Mwenyekiti wa kijiji ambae pia ni mwanajamaat wa hapo yeye alisimama kutoa salaam na Shukurani na pia kumthibitishia Amir sahib kuwa hili eneo na Msikiti huu ni mali yao wanajamaat wa hapo na akamuomba asiwe na Khoufu yoyote juu ya hilo.

Baadae alisimama Mh, Diwani wa Kata ya Kinamapula ambayo kijiji cha Butibu kimo ndani yake, naye baada ya kutoa salaam na shukurani kwa uongozi wa Jamaat Butibu kwa kumualika yeye aliwashauri watu wote waliohudhuria kwamba yote watakayoyasikia hapa wanatakiwa wayazingatie na akawaambia kwamba wakimjua Mungu vizuri ndio watapata mafanikio, na akatumia nafasi hiyo kumuomba Amir sahib aufanyie ukarabati msikiti huo.

Baade pia alisimama M/kiti wa kitongoji ambaye yeye baada ya salam na shukurani alisema kwamba ni Jambo la heshima kufikiwa na Ugeni kama huu. Zamani kabla hatukuwa na mafanikio ya dini ya Kiislaam, lakini baada ya kuingia jumuiya ya Ahmadiyya tumeanza kuona mafanikio makubwa katika dini ya Kiislam, hivyo nawaombeni ndugu tuliohudhuria hapa tusikilize kwa makini na tuyazingatie yote yatakayosemwa hapa nina imani yatatusaidia sana.

Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akifungua mmoja ya misikiti wakati wa ziara yake Mkoani Shinyanga.

Baade Amir sahib aliasimama kuzungumza na Wanajamaat wa hapo ambapo baada ya salaam na tashahud na sura Fatiha Amir sahib aliwakaribisha wote na kuwashukuru kwa kuhudhuria.

Amiri sahib aliendelea kusema kuwa ndug zangu nimefurahi sana kwa kuwaona, ni kweli kuwa miezi michache sana iliyopita nilipata habari zenu kuwa mmejiunga na Jamaat na mnaonyesha mapenzi ya dhati kwa Jamaat, hivyo niliweka nia ya kuja mwenyewe kuwatembeleeni na kujionea hali halisi na Alhamdulillah nia yangu hiyo leo imetimia kwa kufika hapa.

Nawaahdi kwamba tutashirikiana wote katika kazi ya kueneza mafundisho ya dini tukufu ya Islaam, kimsingi hilo ndilo jukumu la jamaat ili watu wawe Waislam kwa matendo.

Kumbukeni kuwa kuna mamilioni ya waislaam duniani lakini tofauti yao na sisi ni kuwa sisi tunatakiwa kufuata mafundisho halisi ya Mtume Mtukufu s.a.w, kwahiyo sisi tutajitahidi kutimiza wajibu wetu kwa kuwasidieni ili nanyi muweze kutimiza wajibu wenu.

Ndugu zangu Ahmadiyya imeenea sehemu mbalimbali duniani takriban katika nchi 207 na lengo la Jamaat ni kutufanya kuwa kitu kimoja. Amir sahib aliendelea kuwafahamisha kuhusu Jamaat kama alivyozungumza katika ziara zake za matawi aliyoanzia na mwishowe akawaambia kuwa baada ya kujiunga na Jamaat wanatakiwa wapate mabadiliko ya kweli ili wawe watu wema na kwamba haifai baada ya kujiunga na Jamaat mtu aendelee kuwa na tabia zile zile alizokuwa nazo kabla ya kujiunga na Jamaat.

Pia aliwakumbusha kuwa Mwislamu ni Yule anayesema kwa maneno yake kisha akayatekeleza kwa matendo yake, sisi tunatakiwa kuwa wema na tufanye matendo mema kwani hilo ndilo jukumu letu.

Amir sahib aliwaambia kuwa nimeona mapenzi yenu ya dhati kwa Jamaat na niwahakikishieni kuwa mkiendelea hivi na moyo huu wa mapenzi yenu mema kwa Jamaat basi mtashuhudia

Endelea uk. 10